# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Septemba 28, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580352

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## CCM kutumia mkakati mpya awamu ya tatu ya kampeni

UKURASA 3




UKURASA 11

# Uchaguzi Mkuu 2020 wa kipekee

• **Wachambuzi** watoa tathmini kuutofautisha na uliopita... *Endelea Uk.2*

## Lissu aitwa NEC kujibu tuhuma

UK. 2



Mgombea mwenza wa urais kwa tiketi ya CCM , Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na kuzungumza na wanachama wa chama hicho na wananchi wa Wilaya ya Kiteto katika Kijiji cha Engusero, Dosidosi na Njia Panda Nameroko Kiteto, alipokuwa njiani kuelekea mkoani Manyara jana, kwa ajili ya kampeni. **PICHA: OMR**



Mgombea wa urais kwa tiketi ya ADC, Queen Cuthbert Sendiga (wa tatu kulia), akiwasikiliza baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Kinondoni, katika kampeni za uchaguzi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### YALIYOMO


UKURASA WA 7
**VITUKO VYA WAGOMBEA UCHAGUZI MKUU 2020**


## Mtumishi TRA kortini tuhuma za rushwa

UKURASA 5


Scan Hapa



Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

VOTE

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini

Je ungependa kukishukuru chama chako ?

Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?

Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe MWANGA WA JAMII

VOTE

Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Mgombea mwenza wa kiti cha urais kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Salum Mwalimu (katikati), akisalimiana na Mzee Mohamed Salum, walipokutana katika kijiwe cha kahawa eneo la stendi ya zamani ya mabasi Kondoa mjini juzi jioni, baada ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: FRANCIS DANDE**

# Ni uchaguzi wa kampeni za kistaarabu

**Na Waandishi Wetu**

WADAU wa uchaguzi nchini wametoa tathmini ya mwenendo wa kampeni za uchaguzi mkuu zinazoendelea nchini na kusema vitendo vya matumizi ya lugha za matusi, kejeli na Jeshi la Polisi kutumia nguvu kwa wagombea zimepungua kwa kiasi kikubwa, jambo linalotia matumaini uchaguzi wa Oktoba 28, kufanyika kwa utulivu.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti kuhusu ya tathmini yao ya uchaguzi huu, wadau hao walisema kuwa kampeni za mwaka 2010 na 2015 zilishamiri vurugu katika baadhi ya maeneo, matumizi ya nguvu ya kushusha wagombea jukwaani kulikofanywa na polisi na lugha za matusi zilizotumiwa na baadhi ya wagombea. Walisema kampeni za uchaguzi huu zimeonyesha mabadiliko makubwa na Jeshi la Polisi kuhakikisha wagombea wote wanapata haki sawa.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesom Olengurumwa, alisema uchaguzi huu hakuna vurugu kama ilivyokuwa mwaka 2010 na 2015 jambo linaloonyesha kiwango cha ustaarabu kimeongezeka.

Alisema Jeshi la Polisi linatenda kazi yake vizuri kwa kuwa hadi sasa hakuna matukio ya wagombea kushushwa jukwaani, au wananchi kupigwa na matumizi mengine ya nguvu kupita kiasi, ikiwa ni mabadiliko makubwa ya kiutendaji kwa chombo hicho.

Mchambuzi wa masuala ya kisiasa, Deus Kibamba, alisema kwa ujumla kuna mabadiliko makubwa kwa wagombea kutumia lugha za matusi ingawa baadhi ya wagombea wanawake wametupiwa lugha za matusi ambazo ziliwakatisha tamaa.

Naye Wakili Anna Henga, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), alisema lugha za matusi zilianza mwanzoni mwa kampeni na hasa zilizolenga kushusha thamani ya mwanamke, lakini kwa sasa lugha hizo zimetolewa jambo linaloonyesha watu wamestaarabika.

"Vyombo vya dola (Polisi) wamekuwa wema sana, na hatujaona vurugu zozote ila sehemu chache sana, tofauti na zamani, wagombea kushushwa jukwaani wakizidisha muda, kupigwa na mabomu na machozi. Vimejitahidi sana kutenda haki kwa wagombea wote, hawajaumiza watu na wanawajali wagombea wote," alifafanua.

Naye Wakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar, Othuman Masoud, alisema utendaji wa Jeshi la Polisi ni wa kuridhisha maana hawazuii watu kwenda kwenye mikutano na wanawajibu wa kutenda haki ili mmoja asijione ana haki ya kufanya kosa na hachukuliwi hatua.

Hata hivyo, Olerungumwa alisema dosari ilijitokeza kwenye uteuzi wa wagombea na kwamba katika chaguzi zote imejitokeza kwa mara ya kwanza kuwa wagombea udiwani na ubunge wengi wamekosea kujaza fomu.

Kuhusu usawa kwenye kampeni alisema, vyama vya upinzani vinakabiliwa na ukata jambo linalowafanya washindwe kuwafikia wapigakura na kutoa mapendekezo ya siku zijazo kurejesha ruzuku kwa wagombea, kuruhusu wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuchangia kampeni.

Aidha, alisema ukata umeonekana zaidi kwa kuwa vyama vimeshindwa kuweka mabango ya wagombea katika ngazi zote.

"Tunaposema uchaguzi huru ni pamoja na usawa wa kufanya kampeni, na ndiyo maana kulikuwa na msaada wa kampeni ambazo zilitolewa na serikali ambazo zilifutwa, ingesaidia watu wangekopa na kufanya kampeni na wafanyabiashara walikuwa huru kuchangia vyama vinavyoshiriki uchaguzi kama ilivyokuwa zamani," alisema.

Kuhusu ahadi alisema nyingi ni zile zile za miaka yote za maji, barabara, ajira, ni vitu vinavyo ahidiwa tangu uhuru, na kwamba ni wakati viongozi wawe na fikra tofauti.

Naye, Wakili wa kujitegemea wa Mahakama Kuu Zanzibar, Othuman Masoud, alisema wananchi wengi visiwani humo hawana sifa ya kupiga kura kutokana na changamoto za wakati wa uandikishaji.

"Zanzibar watu wanachotaka ni haki na uchumi mzuri kwa kuwa hali imezidi kuwa ngumu, ahadi nyingi ni nzuri, lakini utekelezaji wake siyo mzuri," alisema.

Naye Kibamba, alisema kuwa kampeni zimepooza na kuwa na mwitikio mdogo wa wananchi kutokana sababu tofauti ikiwamo ukata kwa kuwa kampeni zipo za aina nyingi ikiwamo mabango, vyombo vya habari na magari, zilizopo sasa ni za majukwaani.

"Kampeni hizi kuna mzani haujatulia sababu katika siku 34 kuna baadhi ya vyama havijazindua hata kampeni, ukata unaweza kuwa sababu.

Naye Mchambuzi wa masuala ya siasa, Abulkarim Atiki, alisema kampeni zinakwenda vizuri, tatizo linakuja unapokaribia ndipo joto linapanda na hivyo hali hiyo inabaidi wagombea wajihadhari.

Leo ni siku ya 34 tangu Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), ipulize kipenga cha kuanza kampeni za uchaguzi kwa wagombea udiwani, ubunge na urais, kwa vyama 16 vyenye usajili wa kudumu vilivyosimamisha wagombea.

Vyama hivyo vilianza kwa kuzindua kampeni zake katika mikoa mbalimbali, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kilizindulia jijini Dodoma, Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), CHAUMMA na NCCR Mageuzi vilizindua kampeni zao, jijini Dar es Salaam.

Kadhalika, Chama cha ACT-Wazalendo kilizindua kampeni hizo mkoani Lindi na Chama cha Wananchi (CUF), kilienda kuzindua mkoani Mtwara, huku vyama vya DP, Demokrasia Makini, NRA, SAU, UMD, UPDP, ADC, ADA TADEA, AAFP vikizindua katika mikoa mbalimbali kwa muundo tofauti.

Vyama ambavyo kampeni zake zilizinduliwa kwa kishindo ni CCM, CHADEMA, ACT-Wazalendo, NCCR-Mageuzi na CUF na CHAUMMA.

Vyama vitano pekee ndiyo vimeweka bayana na kusambaza kwenye mitandao ya kijamii ilani zao za uchaguzi kwamba wakipata ridhaa ya kuongoza nchi watawafanyia nini Watanzania katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kitamaduni.

**AHADI ZILIZOTAWALA**

Katika kampeni hizo ahadi kubwa zilizotawala ni kuboresha maisha ya Watanzania, uchumi wa watu, haki, kero ya kodi, vitambulisho vya wafanyabiashara wadogo, mgawanyo wa majimbo, uchumi wa viwanda, kuboresha miundombinu ya maji, barabara, afya, umeme na neema kwa wachimbaji wadogo wa madini.

Nyingine ni ajira, riba ya mikopo ya elimu ya juu, elimu bure, nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma na ruhusa ya kujitoa kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii, pia kuwasaidia wakulima wa mazao ya miti, pamba, korosho na kahawa.

# NEC yamwita Lissu kujibu tuhuma

**Na Waandishi Wetu**

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imemwita kwenye Kamati ya Maadili mgombea urais wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kwenda kujibu tuhuma kwamba Rais Dk. John Magufuli alikutana na wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya majimbo ili kuhujumu uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Akizungumza jana jijini Arusha, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Wilson Mahera, alisema wamemwandikia Lissu barua ya kufika kwenye kamati ya maadili kesho.

Mahera alisema Lissu akiwa Musoma mkoani Mara Septemba 26, mwaka huu, alisikika akisema kuwa Rais Magufuli aliitisha kikao na kukutana na wasimamizi wa uchaguzi wa majimbo yote nchini jijini Dodoma kwa ajili ya kupanga mipango na mikakati ya kuhujumu uchaguzi.

Mbali na tuhuma hizo za Lissu kwa NEC, Mahera alisema Septemba 25, mwaka huu, kuna taarifa zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii zikieleza kuwa Rais Magufuli alifanya kwa pamoja kikao hicho na Mkurugenzi wa NEC na wasimamizi wa uchaguzi majimbo yote.

"Ndugu wananchi na Watanzania wapenda amani, taarifa zote mbili ni za uongo, uzushi na zenye lengo la kuleta taharuki miongoni mwa Watanzania na wapigakura.

"Ili kujenga picha kuwa uchaguzi huu hautakuwa huru na haki na kwamba hata wakishindwa kihalali watataka Watanzania wawaunge mkono kuvuruga amani ya nchi, kwa kuwa wana ajenda zao binafsi," alisema.

Alisema tangu Septemba 25 na 26 mwaka huu, amekuwa akiendelea na ziara yake ya kikazi kukagua na kuratibu maandalizi ya uchaguzi katika majimbo ya mikoa ya Manyara, Arusha na Kilimanjaro.

Aliongeza kuwa katika ziara hiyo, amekutana na wasimamizi wa uchaguzi katika maeneo ya kazi, hivyo tuhuma za Lissu zina lengo baya kwa nchi na kuichafua tume. "Ndiyo maana tumemuita aje kutoa maelezo na ushahidi kwa kile alichokisema.

"Kwa mara nyingine tume inawasihi wagombea wa vyama vyote kufuata sheria, kanuni na taratibu za nchi ili kulinda amani ya nchi katika kipindi hiki cha kampeni kilichobakia."

Pamoja na mambo mengine, NEC imesisitiza wagombea wote kujali muda wa kampeni, ratiba ya kampeni na kuepuka kutumia lugha zisizo na staha na tuhuma zisizokuwa na ushahidi.

Vile vile, alisema kitendo cha baadhi ya wagombea wa urais hususani wa CHADEMA, amekuwa akiikashifu NEC, kwa kusema kuwa itaiba kura zake.

Alisema kitendo hicho ni cha kuidhalilisha tume na kutaka kuitisha ili isifanye kazi zake kwa uhuru suala hilo halikubaliki.

**MAJIBU YA CHADEMA**

Alipotafutwa kuthibitisha kupokea barua hiyo, Meneja wa kampeni wa Lissu, Amani Golugwa, alisema hawajapokea barua hiyo, lakini wakiipokea mgombea wao ataitikia wito kwa kwenda mbele ya kamati.

**KUBORESHA AFYA**

Wakati huohuo, Lissu amesema endapo chama hicho kitachaguliwa, kitahakikisha kinaboresha huduma za afya. Akizungumza katika muendelezo wa kampeni zake katika maeneo mbalimbali ya Butiama na Tarime Vijijini mkoani Mara, Lissu alisema maeneo mengine ambayo chama hicho kitaweka nguvu zake ni pamoja na katika sekta ya kilimo.

Pia alisema chama hicho kimejipanga kusaidia wajasiriamali wadogo kwa kuwawekea mazingira mazuri ya biashara. Lissu alisema wanaamini kwamba uchaguzi utakuwa huru na wa haki.

"Uchaguzi huru maana yake ni kuhakikisha kila chama kinakuwa na mawakala, wanaapishwa na wanaruhusiwa kuingia katika vituo vya kupigia kura na kupewa fomu za matokeo ya kila kituo," alisema Lissu.

"Uchaguzi huru maana yake ni kwamba, wananchi wote waliojiandikisha kupiga kura, waruhusiwe kupiga kura na mshindi halali wa kila kata, jimbo na urais atangazwe."

**Imeandikwa na na Allan Isack, ARUSHA na Elizabeth Zaya, DAR**

# Wastaafu kukoleza moto kampeni CCM awamu ya 3

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kuelekea siku 30 za mwisho za kampeni watakazozianza leo, kitaongeza 'injini' mpya kwa kuwatumia mawaziri wakuu wastaafu, marais wastaafu na makada waandamizi, watakaofanya mashambulizi mapya kila kona ya nchi.

Kimesema mgombea urais wa chama hicho, Dk. John Magufuli atazitumia siku hizo kutoa maelezo yaliyosheheni takwimu sahihi, maono yake kwa Watanzania pamoja na kueleza yaliyomo kwenye ilani ya chama hicho.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Taifa, Humphrey Polepole (pichani), aliyasema hayo jana mjini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu awamu ya tatu ya kampeni za urais wa chama hicho, zitakazoanza leo katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini ikiwamo, Iringa na Mbeya.

"Zitakuwa ni siku 30 kuu, Dk. John Magufuli ataendelea kesho (leo) na mzunguko wake wa kampeni akitokea mkoani Dodoma kuelekea Iringa na njiani atahutubia na kusalimia wananchi, pamoja na kuomba kura zake, madiwani na wabunge," alisema Polepole na kuongeza:

"Akifika Iringa atafanya mkutano mkubwa katika Uwanja wa Samora, kesho yake ataelekea mkoani Mbeya akipitia mkoani Njombe, Makambako nako atafanya mikutano njiani, Septemba 30 atawasili mkoani Mbeya na kufanya mkutano mkubwa," alisema Polepole.

Aliongeza kuwa Dk. Magufuli atazitumia siku hizo kutoa takwimu sahihi kwa kueleza nchi ilipotoka, ilipo na inapokwenda kwa kutumia ilani ya CCM.

Aidha, Polepole alieleza kuwa Dk. Magufuli hatatumia majukwaa kujibizana na wagombea wengine wa vyama vya siasa, bali atajikita katika Ilani kwa kuelezea mustakabari wa Taifa kwa miaka ijayo.

"Watanzania wajiandae kupokea ujumbe wa amani, siku zilizobaki tutaongeza injini mpya katika kampeni, mgombea mwenza, Samia Suluhu Hassan, Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa NEC, Kassim Majaliwa, mawaziri wakuu wastaafu na makada mbalimbali watatumika kushambulia kila kona, tunakwenda kuwamaliza wapinzani," alisema Polepole.

Alisema zitakuwa ni siku 30 za kueleza namna ya kuibadilisha mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Arusha, Pwani, Kilimanjaro, Dodoma na Tanzania yote, kwamba zitakuwa ni siku za maangamizi kwa upinzani.

**AKANUSHA UZUSHI**

Aidha, Polepole alikanusha taarifa zilizotolewa na mmoja wa wagombea urais wa upinzani kwamba Rais John Magufuli amewaita Wakurugenzi wa Halmashauri mjini Dodoma na kufanya nao vikao vya siri.

Polepole alisema: "Ni taarifa za uzushi, uongo zenye kuwafitinisha Watanzania, tunaiomba TAMISEMI watolee ufafanuzi.

**ALAANI MAUAJI**

Wakati huohuo, Polepole alilaani kifo cha Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM, Vyuo Vikuu mkoani Iringa, Emmanuel Mlelwa, anayedaiwa kuuawa na watu wasiojulikana.

Polepole alisema CCM wana taarifa za waliohusika na kifo cha Mlelwa, kulitaka Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi na kuwakamata wote waliohusika na kifo hicho. "Mwili wake ulikutwa eneo la Kibena Bwawani ukiwa umeumizwa na amefariki... nitoe rai kwa Jeshi la Polisi lihakikishe ukweli unafahamika na hatua kali zinachukuliwa kwa wote waliohusika na tukio hilo, kijana huyu alikuwa na ndoto zake," alisema Polepole.



# Ibrahim Lipumba ajinadi kuimarisha elimu, uchumi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MGOMBEA urais kupitia Chama cha Wananchi (CUF), Prof Ibrahim Lipumba, (pichani) ameahidi kuimarisha uchumi, elimu kwa wananchi endapo atachaguliwa kuingia ikulu.

Pia, aliahidi kufanya maboresho katika sekta za kilimo na kuondoa kero mbalimbali zinazowakabili wananchi kwa sasa.

Prof. Lipumba alitoa ahadi hiyo akiwa katika mwendelezo wa mikutano ya kampeni katika Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera.

Alisema mkoa huo una fursa nyingi za kibiashara kutokana na kupakana na nchi nyingi ikiwamo Burundi, Uganda, Rwanda hususani kwa kutumia mazao ya kilimo kuuza katika nchi hizo na kujipatia kipato kikubwa cha kuboresha uchumi wake.



Prof. Lipumba alisema fursa nyingine zilizopo katika mkoa huo ni pamoja na zile zinazotokana na rasilimali za mito na maziwa na kwamba endapo chama hicho kitachaguliwa kitahakikisha kinaweka mifumo bora kwa wananchi wa mikoa hiyo kunufaika na fursa hizo.

"Kuna rasilimali za kilimo, ufugaji samaki ambazo zinapatika hapa na zinatosha kabisa kuwapatia watu wa mikoa hii ya Kanda ya Ziwa kujipatia kipato kwa kushiriki katika masoko ya jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Prof. Lipumba.

Alisema ili kujenga uchumi imara, kuna haja ya kufanya mabadiliko kwa kuhakikisha kunawekwa mfumo bora wa kutoa na kuingiza bidhaa kutoka nchi moja na nyingine kwa kutumia masoko ya pamoja

Prof. Lipumba alisema kuna haja Tanzania kuhakikisha kwamba inatoa kipaumbele kwa ukuaji wa sayansi na teknolojia ikiwamo kwa kuutumia katika shughuli mbalimbali ikiwamo katika sekta ya elimu, afya, na nyinginezo.

"Raslimali watu ya elimu ni uwekezaji unaojiendeleza, nchi nyingi kwa sasa zinatumia TEHAMA kwa ajili ya kuweka mifumo ya wanafunzi kutumia kompyuta na intaneti, hata sisi hapa inawezekana lakini ni lazima kwamba tuwadhamini walimu wetu," alisema Prof. Lipumba.

Mgombe huyo wa CUF, alisema endapo atachaguliwa atahakikisha kwamba anaunda serikali ya umoja wa kitaifa ambayo itawaweka Watanzania wote pamoja bila kujali, dini, rangi na itikadi ya vyama vyao.

Profesa Lipumba alisema katiba mpya ambayo itaandikwa na chama hicho, itajikita katika misingi ya haki kwa makundi yote.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAJI

MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

ewura

**TANGAZO KWA UMMA**

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inawaalika mafundi umeme wote wa mikoa ya Dar es Salaam na Pwani kwenye semina ya siku tatu (3) itakayoanza saa tatu (3) asubuhi, tarehe **30/09/2020** hadi tarehe **02/10/2020.** Semina itafanyikia ukumbi wa Baraza la **Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)** uliopo Mikocheni eneo la Viwanda.

Baadhi ya mambo yatakayofundishwa ni pamoja na namna ya kupima vitu muhimu kama vile earth resistance, insulation resistance na earth loop impedance katika mfumo wa umeme.

**Jinsi ya kufika ukumbini:** ***kutokea Kituo cha basi ITV, fuata barabara inayokwenda Chuo cha Kodi Mikocheni, elekea upande wa kulia.***

Kwa mafundi watakaopenda kuhudhuria wathibitishe ushiriki wao kabla ya tarehe 29/09/2020 kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi **(SMS) 0754 26 59 36 au piga +255222123850/3/4/6.**

**MAFUNZO HAYA NI BURE KABISA**

**Limetolewa na**

**MKURUGENZI MKUU**
**EWURA**

215915402

# Staili za wagombea kuomba kura zawa kivutio

**Na Thobias Mwanakatwe**

KAMPENI za uchaguzi mkuu unaotarajia kufanyika Oktoba 28, mwaka huu, zimeonekana kuweka rekodi mpya ukilinganisha na uchaguzi uliopita kutokana na 'staili' zinazotumiwa na wagombea katika kuomba kura kwa wananchi katika maeneo mbalimbali.

Uchunguzi uliofanywa na gazeti hili katika maeneo mbalimbali ya kampeni umebaini kuwa baadhi ya wagombea kutoegemea mikutano ya hadhara ya kampeni pekee na badala yake wanatumia staili za kusaka kura kwa kuwafikia wananchi kwenye makundi tofauti.

Baadhi ya staili zinazotumiwa na wagombea kuomba kura ni kutembelea vibanda vya mamalishe, saluni za kike, sokoni, kutumia usafiri wa punda na pikipiki.

Miongoni mwa wagombea ambaye amekuwa na ubunifu wa kipekee wa kusaka kura na kuwa kivutio kwa wananchi ni mgombea ubunge Jimbo la Ukonga kwa tiketi ya CCM, Jerry Slaa.

Slaa ameonekana kuomba kura kwa wananchi kwenye saluni za kike na kivutio zaidi ni kushiriki kuwahudumia wateja kwenye saluni hizo.

Katika moja ya picha iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii ameonekana akimhudumia msichana kwa kumtengeneza kucha za miguu kwenye saluni moja huko Jimbo la Ukonga.

Mgombea huyo katika picha nyingine ameonekana akisaka kura kwa kushiriki kupakua chakula kwa wateja kwenye vibanda cha mamalishe na kushona viatu kwa mafundi.

Maoni ya wananchi yanaonyesha kuwa mgombea huyo ndiye anaongoza kwa kuwa staili za kipekee katika kuomba kura kwa wapigakura wa Jimbo la Ukonga.

Mgombea ubunge Jimbo la Temeke kupitia CCM, Dorothy Kilave, naye alionekana kuendesha kampeni kwa staili ya kusuka wateja kwenye saluni za kike.

Mgombea ubunge wa Tarime Vijijini kwa tiketi ya CCM, Mwita Waitara, amekuwa akitumia pikipiki kwa kuendesha mwenyewe kusaka kura kwa wananchi.

Waitara ambaye ni Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, amekuwa kivutio kwa wananchi wa jimbo hilo kwa kuomba kura kwa kuendesha pikipiki.

Kadhalika, staili ya viongozi wa CCM kuomba kura kwa staili ya kuwapigia magoti wananchi, mbunge anayemaliza muda wake wa Viti Maalum Mkoa wa Mbeya, Mary Mwanjelwa, ndiye anayeongoza.

Katika kila jimbo mkoani Mbeya, Mwanjelwa, amekuwa akiwaombea kura wagombea kwa kupiga magoti kuonyesha unyenyekevu kwa wananchi.

Mgombea udiwani Kata ya Segerea kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Marysponsa Mbilinyi naye amekuwa kivutio kwa staili yake ya kuomba kura kwa mam lishe, waendesha pikipiki (bodaboda) na saluni.

# Mgombea ataka aweke historia urais

**Na Elizabeth Zaya**

MGOMBEA urais wa kupitia Chama cha Alliance for Democratic Party (ADC), Queen Sendiga, amewaomba Watanzania kumchagua ili awe rais wa kwanza mwanamke na kuingia katika historia, huku akiahidi kufanya mageuzi makubwa katika sekta mbalimbali nchini.

Alisema akipata nafasi hiyo atahakikisha anatengeneza mazingira wezeshi ya ajira kwa Watanzania ikiwa ni pamoja na kuimarisha sekta binafsi nchini.

Akizungumza jana katika moja ya mkutano wake wa kampeni jijini Dar es Salaam, alisema ili kuwa na uchaguzi wenye amani ni vyema Watanzania wakatunza tunu hiyo.

Aliahidi kuwa endapo atachaguliwa kushika nafasi hiyo, anajiamini kuleta mageuzi makubwa nchini katika sekta zote zinazogusa maisha ya wananchi.

"Ninajiamini, uwezo nilionao ni mkubwa, Watanzania waniamini, nitasimamia kwa kiwango kikubwa kuweka mifumo bora na imara ya kuliletea maendeleo taifa letu, naomba mnipigie kura," alisema Sendiga.

Kwa mujibu wa mgombea huyo, vipaumbele vyake vitakuwa ni pamoja na kulinda haki za wanawake, watoto na makundi maalum, pia tatizo la ajira kwa vijana.

Sendika ni miongoni mwa wanawake wawili kati ya wagombea 16 kwa upande wa Tanzania Bara ambao wamejitosa katika kinnyang'anyiro cha urais.

Licha ya ukata unaovikabili vyama vingi vya upinzani katika kufanya kampeni, mgombea huyo ameonekana maeneo mbalimbali nchini akinadi sera za chama chake kwa wapigakura.

Mgombea mwingine mwanamke katika nafasi hiyo ni Cecilia Mwanga, kupitia Chama cha Demokrasia Makini.




Mgombea ubunge Jimbo la Ukonga kupitia CCM, Jerry Slaa (kushoto), akimsafisha kucha mteja, akiwa katika kampeni za uchaguzi mkuu, katika Kata ya Ukonga, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yazindua awamu ya tatu kampeni

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimezindua awamu ya tatu ya kampeni huku kikisema hakitakuwa tayari kujibu uchonganisha unaofanywa na wapinzani wao badala yake kimejipanga kuwashinda kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu.

Katibu Mkuu wa Chama hicho, Dk. Bashiru Ally, akizungumza jana wakati wa uzinduzi huo uliofanyika Jimbo la Kongwa, mkoani Dodoma, alisema uchaguzi wa mwaka huu ni wa aina yake kutokana na CCM kushindana na watu waliochoka kisiasa.

"Dawa yao si kuwapuuza ni kuwashinda ili wachague njia tatu, mojawapo ama kuja CCM na tutawapokea kwa sababu ni wenzetu au kustaafu siasa na kuanza kujenga upya vyama vya kitaasisi vitakavyoshindana na CCM," alisema.

Dk. Bashiru alisema, CCM viongozi wamegawana kanda katika kupiga kampeni na kushawishi wananchi wajitokeze kwa wingi katika kupiga kura siku ya Oktoba 28, mwaka huu.

"Makisio yetu hadi leo (jana) CCM ina uhakika wa kushinda kwa zaidi ya asilimia 89 kwa nafasi ya urais, wabunge na madiwani," alisema. Alisema kwa wastani kila siku madiwani, wabunge na wawakilishi wa CCM wanafanya mikutano ya kampeni 600 wakati kampeni za kitaifa zinazoongozwa na mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli na viongozi wengine wanafanya wastani wa mikutano 20 kwa siku. Kwaupande wake mgombea mwenza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alisema ikiwa wananchi watakipa ridhaa chama hicho, kimejipanga kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kukamilisha iliyobaki.

Mama Samia alisema kwa Mkoa wa Dodoma miongoni mwa miradi itakayotekelezwa ni ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato ambao kazi ya usanifu ilishakamilika na inayofuata ni kutafuta mkandarasi ili ujenzi uanze mara moja.

Alisema miaka mitano ijayo, wananchi wakiichagua, Serikali ya CCM, itawakopesha vifaa wanafunzi wanaomaliza vyuo vya ufundi kwa masharti nafuu ili waweze kujiajiri na wao kuajiri wenzao.

Alisema kutaanzishwa programu maalum kwa wanafunzi watakaomaliza elimu ya vyuo vya juu kupatiwa mitaji ili waweze kuanzisha miradi na kujiajiri wenyewe.

HABARI KITAIFA

# Mtumishi wa TRA kortini madai ya kupokea rushwa

**Na Jumbe Ismailly,** NZEGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora imempandisha kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi mtumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wa wilaya hiyo, Dickson Mtandu Mtandu, kwa tuhuma za kuomba rushwa ya Sh. milioni 1.5 kutoka kwa mfanyabiashara wa nyumba ya kulala wageni.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU Wilaya ya Nzega, Mazengo Joseph, alidai, kwamba mtuhumiwa alitenda kosa hilo kinyume cha Kifungu cha 15 (1) (a)(2) na 3(a) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11/2007.

Mwendesha mashtaka huyo alidai mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Nzega, Joseph Mwita, kwamba kati ya Agosti 26, mwaka huu na Agosti 28, mwaka huu kwa nyakati tofauti mshtakiwa akiwa eneo la Mery Pud mjini Nzega, aliomba rushwa ya Sh. 1,500,000 kutoka kwa Sahani Katuli ili asimchukulie hatua za kisheria kwa kutotoa risiti ya EFD katika nyumba yake ya kulala wageni ya Kipozo ilioko mjini Nzega. Aidha, Mazengo alidai pia kwamba Agosti 29, mwaka huu, mshtakiwa alikamatwa na maofisa wa TAKUKURU Wilaya ya Nzega wakati akipokea rushwa ya Sh. 400,000 kati ya Sh. 1,500,000 alizokuwa ameomba kutoka kwa mlalamikaji baada ya kuwekewa mtego na taasisi hiyo.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo baada ya kusomewa shtaka, alikana kutenda kosa hilo, na yupo nje kwa dhamana ya shilingi milioni moja na wadhamini wawili hadi Oktota 20, mwaka huu itakapotajwa.

## Warundi wauawa kwa madai ya ujambazi

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

RAIA wawili wa Burundi, wanaodaiwa kuvamia soko kufanya uhalifu wameshambuliwa na kuuawa na wanakijiji katika tukio ambalo pia, wananchi wengine sita wamejeruhiwa.

Uvamizi huo ulifanywa katika soko la Kijiji cha Kalela wilayani Kasulu mkoani Kigoma. Akithibitisha kutokea kwa tukio hilo Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kigoma, James Manyama, alisema mauaji hayo yalitokea wiki iliyopita saa 1:45 usiku baada ya watu watatu wanaodhaniwa kuwa ni majambazi walipovamia soko la Kalela.

Baada ya uvamizi huo wananchi walitoa taarifa polisi na wakati huohuo wakiwa na silaha za jadi kama fimbo, rungu na mawe waliwashambulia na kuwaua wawili ambao bado majina yao hayajafahamika wakati mmoja kutoroka. Kamanda Manyama alisema katika tukio hilo watu hao wanasadikiwa kuwa ni majambazi waliwafyatulia risasi nyingi wananchi na takribani sita walijeruhiwa na kuepelekwa hospitali wanapoendelea na matibabu

"Kwanza nawapongeza wananchi wa Kalela kwa kuitikia wito wetu wa ulinzi shirikishi na kufanikiwa kuwakamata majambazi hao na kuwadhibiti lakini nitoe rai mnapokuwa mmeshatoa taarifa polisi msijichukulie sheria mkononi ili watu hao wafikishwe katika vyombo vya sharia," alisema.

Aliongeza kuwa baada ya tukio hilo polisi ilikamata silaha ya kivita aina ya AK 47 na maganda ya risasi 45 zilizotumika na nyingine moja ambayo haikutumika.

Aidha, silaha hiyo haina usajili na kwamba wanahusisha tukio hilo kuwa lilitekelezwa kwa ushirikiano wa raia wa Burundi na Watanzania.

Kamanda Manyama alisema wanawashikilia Watanzania watatu kwa mahojiano kuhusiana na tukio hilo na muda wowote uchunguzi ukikamilika watafikishwa mahakamani.

Aidha, Kamanda Manyama amewataka wananchi mkoani Kigoma kujiweka tayari kwa kuanzisha vikundi vya ulinzi shirikishi kutokana na tishio la ujambazi unaofanywa kwa asilimia kubwa na raia kutoka nchi jirani hasa Burundi.

"Tunajua upande wa pili kuna matatizo makubwa, hivyo tunatoa elimu kwa wananchi wawe tayari muda wote kukabiliana na uvamizi," alisema Manyama.

## EPZA, Jiji Dar kupitia maeneo maalum ya uzalishaji

**Na Mwandishi wetu**

MAMLAKA ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji wa Mauzo ya Nje (EPZA), kwa kushirikiana na Mkoa wa Dar es Salaam wamefikia muafaka wa kupitia kwa pamoja maeneo maalum ambayo yatasaidia kusukuma mbele uchumi wa viwanda.

Akiongea wakati wa kufunga mafunzo maalum ya siku moja kwa maofisa wa serikali wanaounda kamati za uchumi na biashara kutoka katika halmashauri za jiji la Dar es Salaam, Katibu Tawala wa Mkoa, Paulo Makanza, alisema kuwa kuna umuhimu wa kuanzishwa maeneo mengi ya viwanda ili kuchangia kusukuma uchumi wa viwanda nchini.

"Tukiendeleza maeneo mengi maalum ya viwanda itasaidia sana kuongeza ajira, mauzo ya nje na kuingizia nchi fedha za kigeni, pamoja na kukuza kwa kasi uchumi wa viwanda," alisema.

Aliwataka wakazi wa Jiji la Dar es Salaam na Watanzania kwa ujumla kutumia fursa hiyo ya kuwapo kwa EPZA na maeneo mbalimbali ya viwanda kujua kwa kina uwekezaji uliofanyika katika sekta ya viwanda nchini na manufaa ambayo yamepatikana hadi sasa.


Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mipango na Maendeleo wa EPZA, Lamau Mpolo, alisema katika malengo ya muda mfupi, mafunzo hayo yatasaidia kuboresha utoaji huduma kwa wawekezaji waliopo na wale wanatarajiwa kuja ikiwa ni matunda ya kufanyika kwa mafunzo kwa maofisa kutoka halmashauri za jiji hilo.

"Kupitia mafunzo haya tunaamini wawekezaji wanaopitia mamlaka ya EPZA na wale wanaopitia taasisi nyingine za serikali watapata huduma bora zaidi na kwa wakati," alisema. Katika malengo ya muda mrefu, alisema EPZA na Jiji la Dar es Salaam wanatarajia kuanzisha maeneo maalum ya uwekezaji bila kujali tofauti ya majukumu ya kila taasisi, lakini wote wakiwa na lengo la kuendeleza maslahi ya serikali kujenga uchumi imara wa viwanda.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kujenga uelewa wa pamoja kati ya taasisi hizo mbili na kuangalia kwa namna gani kila moja inaweza kutoa mchango mkubwa katika uendelezaji wa viwanda nchini.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa anayeshughulikia uzalishaji na uchumi, Dk. Elizabeth Mshote, alisema mafunzo hayo yamewajengea uwezo na uelewa kwa masuala mbalimbali yanayohusu uendelezaji wa viwanda nchini.

"Tumejifunza kwa vitendo kutoka katika mamlaka ya EPZA juu ya majukumu yao na namna ambavyo wanaweza kusaidia katika uanzishaji na ujenzi wa viwanda katika halmashauri zetu za Jiji la Dar es Salaam," alisema.



Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Dk. James Jesse, akishuhudia tukio la wanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi ya Genius Kings' ya Tabata Segerea Dar es Salaam, wakimfanyia upasuaji sungura wakati wa maonyesho ya taaluma kwenye mahafali ya tisa ya darasa la saba mwishoni mwa wiki **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Tani 1,700 za mbaazi zakosa soko

**Na Said Hamdani, LINDI**

TANI 1,700 zao la mbaazi mkoani Lindi zimekaa kwenye maghala kutokana na kukosa wanunuzi, jambo ambalo limewaweka wakulima njiapanda.

Mbaazi hizo ni za wilaya za Nachingwea na Ruangwa na zimehifadhiwa kwenye maghala yanayomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika ununuzi wa mazao (RUNALI).

Mrajisi wa vyama vya ushirika mkoani Lindi, Edmund Massawe, aliyasema hayo wakati akijibu maswali na malalamiko yaliyowasilishwa na wajumbe kwenye kikao cha tathmini ya zao hilo kilichofanyika mjini humo.

Alisema kukosekana kwa wanunuzi tani 1,700 za zao la mbaazi kati yake 540 zipo maghala ya wilayani Ruangwa.

Massawe alisema wapo baadhi ya wanunuzi walijitokeza kutaka kununua mbaazi hizo kwa bei ya Sh. 400 kwa kilo kwa masharti ya kutolipa aina yeyote ya ushuru ukiwamo ule wa Serikali za Mitaa jambo ambalo kimsingi limekuwa gumu kukubalika.


**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**BARNABAS AMBROSS UISSO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA HILUX YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 493 AGD.** CHASSIS NAMBA **YN1060002256.** ENGINE NAMBA **4Y0261680.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **WNB/RB/1081/2020.**

115918302

**KUPOTEA KWA CHETI**



115918102

**GREGORY GABRIEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0616-0055** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWANDIGA SEKONDARI November, 2000. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KIG/KIG/RB/686284/2020.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**MARLON GREEN MWASAKANDU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 703 DGF.** YOYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **MBE/KYE/RB/670187/2020.**

115918202

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ubora wa ligi unaonekana, TFF sasa isilale kwa waamuzi

**MZUNGUKO** wa nne wa Ligi Kuu Bara unatarajiwa kukamilika leo kwa Coastal Union ya Tanga kuikaribisha JKT Tanzania katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, baada ya timu zingine 16 kukamilisha raundi hiyo kuanzia Ijumaa, Jumamosi na jana Jumapili. Hadi ligi hiyo inafikia hatua hiyo, Azam FC ndiyo iliyopo kileleni baada ya kushinda michezo yake yote minne ikianza kwa kuichapa Polisi Tanzania bao 1-0 kisha wakaifunga Coastal Union mabao 2-0, ikafuata Mbeya City iliyopigwa 1-0, kabla ya Jumamosi kukamilisha raundi ya nne kwa kuinyuka Tanzania Prisons 1-0.

Pia hadi kufikia mzunguko huo wa nne, Azam FC ndiyo timu pekee ambayo haijaruhusu bao lolote kwenye wavu wake, licha ya kwamba ushindi wake mkubwa ni wa mabao 2-0 tu, tangu imeanza msimu huu.

Lakini pia mpaka ligi hiyo inafikia mzunguko huo wa nne, Mbeya City ndiyo timu iliyopoteza mechi zote nne kabla ya matokeo ya Mwadui FC, ambayo nayo ilipoteza michezo yake mitatu ya nyuma, lakini ikitarajiwa pengine ingefuta balaa hiyo dhidi ya Ihefu FC kwenye Uwanja wao wa Mwadui Complex mjini Shinyanga jana. Aidha, hadi kufikia hatua hiyo kabla ya mechi za jana, ushindi mkubwa uliopatikana ni Simba dhidi ya Biashara United ilipoichapa mabao 4-0, kisha ikashinda 3-0 dhidi ya Gwambina FC, lakini KMC FC ikiichapa Mbeya City 4-0 na Polisi Tanzania ikishinda 3-0 dhidi ya Dodoma Jiji.

Ikumbukwe kabla ya mechi za jana, tayari michezo 32, ilishachezwa, lakini ukiacha ushindi huo mkubwa wa Simba na KMC, ni mechi nne tu zilizotoa matokeo ya mabao mawili, ambazo ni Simba ikishinda 2-1 dhidi ya Ihefu FC, Azam FC ikiichapa Coastal Union 2-0, JKT Tanzania ikilala 2-0 dhidi ya Dodoma Jiji, KMC ikiibuka na ushindi wa 2-1 dhidi ya Prisons na kisha ikapata matokeo kama hayo dhidi ya Mwadui FC. Matokeo ya mechi zingine zote zilizosalia yakawa ushindi wa bao 1-0, sare ya 1-1 ama suluhu, jambo ambalo linaonyesha msimu huu wa 2020/21, unaelekea kuwa kati ya misimu migumu zaidi katika historia ya ligi hiyo tangu ianze kuchezwa kwa utaratibu wa msimu kutoka ule wa kila mwaka.

Hata hivyo, hadi sasa hapajawa na malalamiko makubwa ya waamuzi kuvurunda kama ilivyokuwa msimu uliopita, ambapo timu nyingi zilianza ligi hiyo kwa kuwatupia lawama za kubinywa kwa sheria 17 za soka mpaka msimu unamalizika kwa Simba kuwa mabingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

Tunatambua yapo makosa madogo ambayo tayari yamefanywa na waamuzi pamoja na wasaidizi wao, lakini mengine ni ya kibinadamu na si ya kukusudia kama ambavyo baadhi ya mashabiki wameanza kufungua midomo yao kwa kupaza sauti.

Tunaamini hatua ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), kupitia Bodi yake ya Ligi (TPLB), kukubaliana na wadhamini wao wenye haki ya kurusha matangazo ya mechi hizo kwa kuzionyesha zote mubashara, kumechangia kwa asilimia kubwa kupunguza tabia ya baadhi ya waamuzi wasiowaaminifu, kufuata sheria 17 ipasavyo. Lakini, katika hilo hatuna budi kuitaka TFF kupitia TPLB, kuendelea kuwamulika zaidi waamuzi wafinyangaji wa sheria 17 za soka kwa kuwachukulia hatua kali zaidi ili kuufanya ubora ambao Ligi Kuu imeanza nao msimu huu, kuendelea kuonekana na hata kuongezeka hadi mwishoni mwa msimu. Ni wazi, hatua ya nchi kama Ghana ambayo imesheheni wachezaji wengi wanaocheza soka la kulipwa Ulaya na kila kona katika mataifa yalisonga mbele kisoka, kumulika Ligi Kuu Bara, na kisha kumuita timu ya taifa mchezaji wa Azam FC, Mghana Yakubu Mohammed, ni ushahidi kwamba ligi yetu imekua na inafuatiliwa zaidi nje na ndani ya bara la Afrika.

Si Yakubu pekee, bali Claotus Chama, Rally Bwalya wa Simba, Obrey Chirwa wa Azam wote hao wameitwa timu ya Taifa ya Zambia, lakini Luis Miquissone akiitwa kuitumikia Msumbiji, hii yote inamaanisha tunapaswa kuwa na waamuzi bora zaidi ambao wanatenda haki kwa kufuata sheria 17 za soka ili kuifanya ligi yetu kuzidi kuwa bora zaidi, hivyo TFF na TPLB hawapaswi kulala katika kuwashughulikia wale wote wanaozifinyanga sheria hizo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

Na Nebart Msokwa

# Mbeya City kujinasua mkiani 'dabi' ya Mbeya Jumamosi?

**LIGI** Kuu ya Vodacom Tanzania Bara Msimu wa 2020/21 inayoshirikisha timu 18 imefikia mzunguko wa nne kwa kila timu kushuka dimbani mara nne.

Mbeya City ambayo ni miongoni mwa timu tatu za Mkoa wa Mbeya zinazoshiriki ligi hiyo pamoja na timu za Ihefu FC na Tanzania Prisons ambayo kwa sasa wamehamia mkoani Rukwa wakitumia Uwanja wa Nelson Mandela kama dimba lao la nyumbani.

Tangu msimu huu ulipoanza, Mbeya City ni timu ambayo imeonekana kuwa kibonde kuliko timu nyingine yoyote ambapo mpaka sasa imecheza michezo minne na kupoteza yote.

Mpaka sasa timu hiyo inaburuza mkia kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa haina alama na ndiyo timu inayoongoza kwa kufungwa magoli mengi ambapo mpaka sasa nyavu zake zimetikiswa mara saba.

Mbali na kuongoza kufungwa magoli mengi, pia Mbeya City ni miongoni mwa timu tatu ambazo hazijafanikiwa kupata bao hata moja kwenye michezo yote minne iliyocheza.

Mechi ya kwanza Mbeya City walikubali kupokea kichapo kizito cha mabao 4-0 kutoka kwa watoza ushuru wa Manispaa ya Kinondoni timu ya KMC ya jijini Dar Es Salaam kwenye mchezo namba saba uliopigwa Uwanja wa Uhuru.

Baada ya hapo wagonga Nyundo hao wa Jiji la Mbeya walipokea kichapo kingine cha bao 1-0 kutoka kwa timu ya Wananchi, Yanga kwenye Uwanja wa Mkapa ambao ulikuwa mchezo wa pili wa timu hiyo kucheza ugenini.

Mtazamo wa wengi ulikuwa ni kwamba timu hiyo ilipoteza michezo hiyo kwa sababu ya kuwa ugenini na hivyo mashabiki na wapenzi wengi wa timu hiyo walitarajia mabadiliko kwenye michezo ya nyumbani.

Hata hivyo, mambo yalienda ndivyo sivyo baada ya Septemba 20 timu hiyo ikicheza mchezo wake wa kwanza nyumbani kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine dhidi ya 'Waokamikate' wa Chamazi, Azam FC walikubali kupokea kichapo cha bao 1-0.

Katika mechi hiyo ambayo ilikuwa ya kwanza kwa Mbeya City kucheza wakiwa nyumbani, walionyesha mchezo mzuri hali ambayo ilianza kufufua matumaini kwa mashabiki wake, lakini wakaghadhabishwa na baadhi ya maamuzi ya mwamuzi wa mchezo huo, Jackson Samwel kutoka mkoani Arusha wakidai alikuwa anaibeba Azam.

Moja ya matukio waliyokuwa wanayalalamikia mashabiki hao ni mshambuliaji wa timu yao, Kibu Denis, kutembezewa kiatu kwenye eneo la hatari wakiamini ilipaswa kutengwa mkwaju wa penalti, lakini mwamuzi aliamuru ipigwe kona.

Mashabiki hao walifanya vurugu ikiwamo kurusha chupa uwanjani wakati mchezo huo ukiendelea na baada ya mchezo huo kumalizika waliendelea kuwatafuta waamuzi ambapo Jeshi la Polisi likaingilia kati kwa kuwatorosha waamuzi hao.

Vurugu hizo zilisababisha timu hiyo ya Mbeya City, kupigwa faini ya Sh. 500,000 na Kamati ya Uendeshaji na Usimamizi wa Ligi ya Bodi ya Ligi Kuu Tanzania Bara (TPLB).

Uwezo mzuri wa Mbeya City kwenye mchezo dhidi ya Azam, uliwavutia mashabiki wengi kujitokeza kwenye mechi yao ya Ijumaa dhidi ya 'Walimakorosho' kutoka Ruangwa mkoani Lindi, Namungo FC.

Pamoja na kujitokeza kwao kwa wingi, kama kawaida "la kuvunda huwa halina ubani", kwani wakati timu yao ilipokubali kipigo cha bao 1-0 kwenye uwanja wao wa nyumbani, wakatoka uwanjani hapo vichwa chini.

Baadhi ya mashabiki hao walijaribu kutaka kufanya tena fujo kwa kuingia uwanjani mchezo ukiwa unaendelea, lakini wakadhibitiwa na viongozi wa timu hiyo.

Baada ya vichapo hivyo, sasa mechi inayofuata nyumbani ni 'dabi ya Mbeya' dhidi ya mahasimu wao, Tanzania Prisons itakayopigwa Ijumaa wiki hii. Je, Kocha Mkuu wa Mbeya City, Amri Said, ataanza rasmi ligi kwa kuibuka na ushindi ama angalau sare katika dabi hiyo? Ni suala la kusubiri kuona.

Hata hivyo, Mbeya City inakwenda kukutana na Prisons ambayo msimu huu imeonyesha kandanda safi na la kuvutia licha ya kupoteza michezo yake miwili kati ya minne ambayo imeshacheza hadi sasa.

Prisons ambayo ipo nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama nne, imeshinda mechi moja na kushinda mmoja, lakini imeruhusu nyavu zake kutingishwa mara nne tu huku washambuliaji wake wazifumania zile za wapinzani mara tatu, hakika itakuwa 'dabi' ya kibabe na ya kuvutia zaidi.

# VITUKO VYA KAMPENI ZA UCHAGUZI MKUU



Mgombea ubunge Jimbo la Ukonga, Jerry Slaa (kulia), akisaidia kusafisha viatu kwa 'shoe shiner' wakati wa uzinduzi wa kampeni za uchaguzi mkuu katika Kata ya Kitunda, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Arusha, Agatha Msuya, akiomba kura za rais, diwani na mbunge, katika mkutano wa kampeni uliofanyika Kata ya Oloirieni, wilayani Arumeru Magharibi, mwishoni mwa wiki. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**



Mgombea udiwani wa Kata ya Kihanga kwa tiketi ya Chama cha Wananchi (CUF), Anastella Kibake, akiwa amepiga magoti kumwombea kura mgombea urais kwa tiketi ya chama hicho, Prof. Ibrahimu Lipumba (kulia), katika mkutano wa hadhara wa kampeni za uchaguzi mkuu uliofanyika katika uwanja wa Changalawe, uliopo mjini Kayanga wilayani Karagwe, mkoani Kagera mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Mgombea wa udiwani Kata ya Kivukoni kwa tiketi ya CCM, Sharik Choughule, akiomba kura kwa wananchi kwa kupiga magoti katika eneo la Feri, jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Mgombea ubunge wa Jimbo la Iringa Mjini kwa tiketi ya Chama cha NCCR-Mageuzi, Robert Kisinini, akihutubia mkutano wa kampeni huku akiwa juu ya mkokoteni unaokokotwa na punda, katika eneo la soko kuu la mji huo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**



Katibu Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Arusha Mjini, Abraham Mollel, akimsaidia mchuuzi kuchambua mboga katika eneo la Kimandolu, jijini Arusha mwishoni mwa wiki, kama sehemu ya kampeni za uchaguzi mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

## Msako waja wachezea mizani

**Na Mwandishi Wetu,** TABORA

WAKALA wa Vipimo Nchini (WMA), unatarajia kufanya msako kuwabaini wafanyabiashara wanaochezea mizani ili kuwapunja wateja wao.

Onyo hilo lilitolewa mwishoni mwa wiki na Ofisa Vipimo wa WMA, Anyitike Tumaini, wakati wa maadhimisho ya wiki ya viziwi kitaifa mkoani Tabora baada ya Umoja wa Miradi kwa Viziwi Tanzania (UMIVITA), kuomba kupewa elimu kuhusu vipimo.

Maadhimisho hayo yalienda na utoaji wa elimu kwa umoja huo ambao alisema kwa muda mrefu makundi ya watu wenye ulemavu yamekuwa yakisahaulika kupata elimu mbalimbali hususani elimu ya vipimo ambayo ina umuhimu katika maisha ya kila siku ya mwananchi.

Tumaini alisema, WMA inasimamia vipimo vyote nchini kwa mujibu wa sheria ili kuhakikisha vinapima kwa usahihi na bidhaa zinazouzwa ziko sahihi na wanaochezea mizani wajue siku zao zinahesabika.

“Lengo kuu la kusimamia usahihi wa vipimo ni kumlinda mlaji asipunjwe kutokana na vipimo na kuhakikisha anapata bidhaa kwa usahihi kulingana na thamani ya pesa yake, hivyo mnapoona mizani imechezewa toeni taarifa tuje mara moja,” alisema.

Tumaini alisema, WMA inahakiki vipimo vyote vinavyotumika kwenye biashara na huduma mbalimbali kama vile afya, usalama na mazingira.

Alisema lengo ni kulinda jamii dhidi ya madhara yatokanayo na matokeo ya upimaji usio sahihi, kuhifadhi usahihi wa vipimo toka vipimo vyenye usahihi wa chini hadi vyenye usahihi wa ngazi ya kati na kusimamia matumizi sahihi.

## Kijiji chahakikishiwa umeme, maji

**Na Francis Godwin,** IRINGA

SERIKALI ya Wilaya ya Kilolo imewahakikishia wananchi wa kijiji cha Ibofwe, kuwa kero ya umeme na maji inayowakabili itashughulikiwa mapema iwezekanavyo kupitia mipango ya serikali ya kusogeza huduma hizo kwa wananchi.

Mkuu wa Wilaya ya Kilolo, Asia Abdallah, aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wake wa hadhara wa kuhamasisha shughuli za maendeleo katika kata hiyo.

Alisema, serikali imesogeza umeme na maji katika maeneo ya vijiji wilayani humo ambavyo awali havikuwa na huduma hizo.

Aliwataka wananchi kuendelea kushiriki katika shughuli za kimaendeleo huku wakiamini kuwa kero zao serikali inazitambua na itazifanyia kazi wakati wowote.

Kadhalika, alisema ushiriki wa shughuli za kimaendeleo kwa wananchi ni hiari na sio vyema kwa viongozi wa vijiji na kata kutumia nguvu kuwalazimisha wananchi kushiriki michango kwa kuwa wananchi pamoja na kuwa na wajibu wa kujitolea katika shughuli hizo haipaswi nguvu kutumika.

Katika hatua nyingine, amepiga marufuku wazazi kuwaruhusu watoto wao kwenda mijini kufanya kazi za ndani badala ya kuwapeleka shule.

Alisema, serikali imelenga kuona watoto wote wanapata elimu ya msingi hadi sekondari bila malipo na hivyo si vyema kuwapo mtu anayekwamisha jitihada hizo.

Aliagiza kila mzazi au mlezi mtoto wake anapata elimu na anasimamiwa vyema bila kukatishwa masomo kwa kumgeuza kuwa sehemu ya watafutaji wa fedha za familia.

# NCC: Epuka rushwa, tatua migogoro

**Na Mwandishi Wetu**

WASULUHISHI wa migogoro ya kibiashara nchini na wahitimu wa mafunzo ya utatuzi wa migogoro ya kibiashara, wameonywa kuhusu rushwa na kutakiwa kuwa chachu ya usuluhishi wenye mafanikio, kwa faida ya biashara zao na uchumi wa taifa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wakitoa mafunzo kuhusu mbinu bora za kutatua migogoro ya kibiashara kwa washiriki wa mafunzo hayo Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, waelimishaji wabobezi wa masuala ya usuluhishi, chini ya Mpango wa Mafunzo wa Baraza la Ujenzi la Taifa (NCC) walisema, rushwa ni kikwazo.

Waelimishaji hao, Mhandisi Samwel Msita na Wakili Rosan Mbwambo, walitoa elimu hiyo ya siku tatu Jumatano iliyopita na kuwataka washiriki wa mafunzo kuzingatia maadili, miongozo, sheria, kanuni na miiko ya usuluhishi, huku wakilenga kuimaliza kwa amani ili biashara zisikwame.

Msita alisema: “Ukiwa msuluhishi mpenda fedha utajikuta ukiuendeleza mgogoro badala ya kuumaliza, kwa sababu hutasimamia haki. Nawasihi wapenda hela kuwa makini na rushwa”.

Alisema ni vyema wakati wowote wanapohitajika kutatua migogoro ya kibiashara, hata kama ni kwenye biashara zao, wasimamie haki na kuangalia namna bora ya kuzifanya pande zilizoingia kwenye mgogoro kuelewana na kuendeleza biashara.

Alisema katika biashara kuna kodi ya nchi inayopaswa kulipwa, hivyo wasuluhishi lazima wawe makini kuhakikisha kupenda kwao fedha hakuwapeleki kuithamini rushwa na kuitengenezea mazingira ya ushindi zaidi ya kutatua migogoro iliyombele yao.

“Ikiwa ni kwenye eneo la manunuzi, msuluhishi zingatia sheria za manunuzi na wala usilete zakwako au kuzipindisha zilizopo kwa faida yako. Tunachokitaka ni kuona unafikiwa muafaka wenye mafanikio,” alisisitiza Msita.

Kwa upande wake, Wakili Mbwambo alisema, siku zote msuluhishi wa mgogoro wa kibiashara anapaswa kuepuka rushwa na sababu nyingine zinazoweza kumfanya abadili kanuni, sheria na miiko ya usuluhishi, kuepuka kupendelea upande mmoja.

Kwa mujibu wa Mbwambo, migogoro ya kibiashara inaposhindwa kumalizwa inazuia wahusika kuendelea kufanya biashara, hivyo wasuluhishi wanapaswa kuhakikisha wanawapatanisha huku kila upande ukipata haki yake unaoidai bila mivutano inayopoteza muda.

Kwa mujibu wa Mbwambo, lengo la usuluhishi wa kibiashara ni kuwaacha walio kwenye mgogoro wa kibiashara wakiwa marafiki wenye uwezo wa kuendeleza biashara kwa amani na kuchangia kukuza uchumi wa nchi.

Mafunzo hayo ya 14 kuandaliwa na NCC yalihusisha washiriki kutoka katika fani mbalimbali ikiwamo biashara, sheria, ujenzi na nyinginezo.




Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati wa Zanzibar, Salama Aboud Talib, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa ushirikiano kati ya Zantel na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), ili kuwawezesha wateja kulipia ankara za maji kirahisi zaidi kwa njia ya Ezypesa, iliyofanyika mjini Zanzibar mwishoni mwa wiki. Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Al-Khalil Mirza na Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA, Mussa Haji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# EWURA kutoa mafunzo kwa mafundi umeme

**Na Beatrice Moses,** TUDARCO

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeshauriwa kuielimisha jamii kuwatumia mafundi umeme waliosajiliwa na taasisi hiyo, ili kuwezesha kazi hizo kufanywa kitaalamu na kuzuia kuzuka kwa majanga ya moto.

Mhandisi Ruta Kasabalala, alitoa tahadhari hiyo juzi wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu mafunzo maalum yaliyoandaliwa na EWURA kwa ajili ya mafundi umeme wa jijini Dar es Salaam na mkoani Pwani.

Kasabalala alisema ni muhimu kwa kuwa yanasaidia kukumbusha au kuwajengea uwezo zaidi mafundi hao kuhusu wajibu wao katika utendaji wa kazi zao.

“Pamoja na nia njema ya EWURA katika kutoa mafunzo haya, wanatakiwa pia kubeba jukumu la kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutumia mafundi umeme waliosajiliwa, kwa kuwa hiyo itasaidia kupunguza majanga ambayo yamekuwa yakizuka, yanawezekana hutokana na ufungaji mbaya wa mfumo wa umeme kwenye majengo mbalimbali,” alisema Mhandisi Kasabalala.

Pia, alisema hatua hiyo itasaidia kuweka thamani ya kazi hiyo ya ufundi umeme kuwa ya kitaaluma na itasaidia kuwachochea mafundi wasiosomea ufundi na kufanya kwa uzoefu kuona umuhimu wa kwenda vyuoni ili kujifunza rasmi, waweze kupata vigezo vya kusajiliwa.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka EWURA mafunzo hayo ya siku tatu yanatarajiwa kuanza Septemba 30 hadi Oktoba 2, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Akifafanua kuhusu mafunzo hayo, Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, alisema mafunzo hayo yanatolewa bure, hivyo mafundi umeme wanaopenda kuhudhuria wametakiwa wathibitishe ushiriki wao kabla ya Septemba 19, mwaka huu.

# Wanaonunua vitambulisho vya kupigia kura waonywa

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MSIMAMIZI wa uchaguzi wa Jimbo la Sumbawanga Mjini, Jacob Mtalitinya, amewaonya watu wanaopita mitaani na kununua kadi ya mpigakura kutoka kwa wananchi, waache mara moja.

Amesema kufanya hivyo ni kosa kwa mujibu wa sheria na atakayebainika atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Onyo hilo alilitoa wakati akitoa taarifa ya mwenendo wa matayarisho ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu. Alisema kumekuwapo na taarifa kuwa baadhi ya watu wanaonekana mitaani wakipita pita na kuwalaghai wapigakura waliopo kwenye orodha ya watu watakaopiga kura mwaka huu na kuwataka kuwauzia vitambulisho vyao, kitendo ambacho ni kosa na atakayebainika atachukuliwa hatua za kisheria.

"Niwatahadharishe kabisa wapigakura wenye kadi za kupigia kura, msithubutu kuuza kadi zenu, wanao nunua kadi hizo wanafanya kosa la sheria, hata wewe unayeuza pia unatenda kosa kwa mujibu wa sheria, angalia usije jikuta unafikishwa mahakamani kujibu tuhuma zitakazo kukabiri," alisema. Pia aliwataka wakazi wa Jimbo la Sumbawanga Mjini kujitokeza kwa wingi siku ya uchaguzi mkuu, ili wakamchague kiongozi atakayefaa kuwatumikia na waepuke ushabiki kwani hivi sasa wanakwenda kuamua hatima ya maisha yao na watoto wao.

Naye Ofisa Uchaguzi wa jimbo hilo, Endrew Zumba, alisema mwenendo wa uchaguzi uko vizuri, kwani hakuna changamoto yoyote iliyojitokeza na wagombea wanaendelea na kampeni zao kwa mujibu wa ratiba.

Alisema vyama vitano vyenye wagombea katika ngazi ya ubunge vimeshazindua kampeni zao isipokuwa DP ambacho nacho kitazindua wakati wowote.



Mkandarasi akiendelea na kazi ya ukarabati mkubwa wa barabara ya Shekilango hadi Bamaga, Manispaa ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shule Kisarawe zapigwa jeki mabati ya mil. 17/-

**Na Futuna Selemani,** KISARAWE

SHULE tatu za msingi wilayani Kisarawe mkoani Pwani zimepewa msaada wa mabati 565 yenye thamani ya Sh. milioni 17 kwa ajili ya kuwawekea wanafunzi mazingira mazuri ya kusomea.

Msaada huo ulipokelewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, kutoka kwa Benki ya NMB na kumkabidhi Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo.

Hafla hiyo ilifanyika katika Shule ya Msingi Chanzige, mjini Kisarawe, huku shule zilizonufaika na msaada huo zikiwa ni Shule ya Msingi Kurui Chole, Msegamo na Kidugalo zilizoko Maneromango wilayani humo.

Viongozi wengine walioshudhuria ni Katibu Tawala Kisarawe, Mwanana Msumi, Ofisa Elimu ya Msingi, Shomari Bane, huku NMB ikiwakilishwa na Meneja wa Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper na Meneja wa Tawi la Kisarawe, Justina Kikuli.

Akizungumza wakati akipokea mabati hayo, Waziri Jafo aliipongeza Benki ya NMB kwa namna inavyoacha alama kwa jamii, kutokana na misaada inayotoa katika vijiji, kata, tarafa, wilaya na mikoa mbalimbali nchini kupitia Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii.

Jitihada kubwa zinafanywa na Serikali ya Rais John Magufuli, lakini bado inahitaji kuungwa mkono na wadau kama ifanyavyo NMB. Benki hii imeacha alama njema kila kona ya Tanzania kwa namna inavyojitoa katika utatuzi wa changamoto za jamii.

"Serikali inatumia zaidi ya Sh. bilioni 23.86 kwa mwezi kuhudumia shule zetu kupitia Sera ya Elimu Bure, sio tu kusomesha watoto bila ada, bali pia kujenga na kukarabati miundombinu, jitihada ambazo zinapaswa kuungwa mkono na wadau kama hawa,» alisema Jafo.

Naye Kaimu Ofisa Mkuu wa Fedha wa NMB, Benedict Baragomwa, alibainisha kuwa, Shule ya Msingi Kurui Chole imepewa mabati 200, Shule ya Msingi Kidugalo mabati 200, huku Shule ya Msingi Msegamo ikipokea mabati 165, yote yakiwa na tahamani ya Sh. milioni 17, ambazo ni sehemu ya asilimia moja ya faida yao kwa mwaka.

"Msaada huu ni sehemu ya utaratibu wetu wa kurejesha kwa jamii asilimia moja ya faida yetu kwa mwaka, ambapo mwaka huu tulitenga Sh. bilioni 1, ambayo inaendelea kutatua changamoto katika sekta za elimu, afya na majanga," Baragomwa.

Kwa upande wake, DC Jokate, alimpongeza Waziri Jafo, ambaye ni Mbunge wa Kisarawe aliyemaliza muda wake na sasa akiwania tena, kwa namna anavyojitoa katika kuleta maendeleo wilayani mwake na kwamba wananchi wanapaswa kujivunia uwepo wake.

# Corona yashusha huduma za chanjo

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa ugonjwa wa corona umechangia kushuka kwa huduma za chanjo hapa nchini.

Kushuka kwa chanjo kulitokana na baadhi ya wazazi na walezi kushindwa kuwapeleka watoto kliniki kupata chanjo wakihofia kupata ugonjwa wa corona.

Hayo yalibainishwa jijini Dar es Salaam na Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Dk. Ayubu Kibao, wakati wa ufunguzi wa semina ya chanjo kwa waandishi wa habari.

"Baada ya kugundulika kunaugonjwa wa corona nchini, wazazi na walezi walishindwa kuwapeleka watoto kliniki kupata chanjo kuhofia wanaweza kupata maambukizi ya ugonjwa wa corona," alisema.

Aliongeza kuwa hata chanjo ambazo zimekuwa zikitolewa shule kwa wanafunzi nazo zilishuka kwa asilimia 48 kutokana na ugonjwa huo, ambapo watoto walikuwa likizo majumbani.

Dk. Ayubu alisema kila mtoto anayo haki ya kupata chanjo na wasichana walio shule wenye umri unaoruhusiwa kupata chanjo wanatakiwa kupata chanjo, ili kuwalinda na ugonjwa wa saratani ya shingo ya kizazi.

Alisema serikali imenunua magari na kusambaza katika halmashauri zote ili gari hizo zitumike kusambaza chanjo.

"Shilingi bilioni 7 zimetumika kununua magari 74 hapa nchini kwa ajili ya kutoa huduma za chanjo nchini," alisema.

Aliongeza kuwa kununuliwa kwa magari hayo kutasaidia kuendelea kusambaza kwa huduma ya chanjo nchini.

# RC ataka vikundi vya mazingira shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Mhandisi Evarist Ndikilo, ameziagiza shule zote za msingi katika mkoa huo kuhakikisha wanaanzisha vikundi vya mazingira vitakavyowaandaa wanafunzi wakiwa na umri mdogo.

Ndikilo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki aliposhiriki maadhimisho ya wiki ya mazingira yaliyofanywa na Shule ya Msingi Mtakatifu John Bosco iliyopo Tumbi Halmashauri ya Mji wa Kibaha.

Alisema, endapo vikundi hivyo vitaanzishwa, vitasaidia kuwaandaa wanafunzi kuwa watunzaji wa mazingira wakiwa na umri mdogo.

Ndikilo alipongeza shule hiyo kwa kufanya maadhimisho hayo kushirikisha wanafunzi ambao watakuwa mabalozi wazuri kwa wazazi wao na jamii inayowazunguka katika suala la utunzaji wa mazingira.

Alitoa rai kwa kila mmoja kushiriki kulinda mazingira ikiwamo kuacha kukata miti ovyo kuepuka athari na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo kukosa mvua kwa wakati na joto kali.

Mkurugenzi wa shule hiyo, Padri Benno Kikudo, alisema, chimbuko la maadhimisho hayo ni waraka kutoka kwa Papa Francis uliotoka mwaka 2015.

Fr Kikudo alisema, wameona waraka huo usibaki katika maono ya kikanisa pekee badala yake wameamua ifike kwa watoto kwa kuwaelimisha kwani wao ndio watakaokuwa kiini cha baadaye kusambaza elimu kwa vitendo.

## Wazazi watakiwa kuwekeza bima ya elimu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZAZI nchini wameshauriwa kujenga utamaduni wa kuwakatia watoto wao bima ya elimu itakayowahakikishia uhakika wa kupata elimu bora hata pale wazazi wanaposhindwa kutimiza wajibu huo kutokana na sababu mbalimbali.

Miongoni mwa sababu hizo imetajwa kuwa ni ya ulemavu wa kudumu au kifo.

Wito huo ulitolewa na Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa wateja wadogo na wa kati wa benki ya NBC, Mussa Mwinindaho, alipokuwa akizungumza kwenye mahafali ya 16 ya Shule ya Msingi Tusiime jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki.

"Bima ya Elimu itawawezesha wazazi kuwa na uhakika na elimu ya watoto wao kwa kuwa mtoto ataweza kusoma kwa kipindi chote cha masomo yake hadi atakapomaliza hata kama wazazi watapatwa na majanga yanayoweza kusababisha ulemavu wa kudumu au kifo," alisema.

Akitolea mfano wa bima ya elimu ya Educare inayotolewa na benki hiyo, Mwinindaho alisema kupitia huduma hiyo mzazi humwekea akiba mtoto wake kidogo kidogo kwa ajili ya elimu kwa kiasi atakachopanga kwa mktaba wa muda kuanzia miaka saba hadi 18, ili kugharamia elimu ya mtoto wake.

Aliongeza kuwa uwekezeji katika elimu ya mtoto ni jambo pekee katika kuhakikisha malengo ya kielimu ya mtoto yanatimia huku pia akitumia fursa hiyo kuwahimiza wahitimu na wanafunzi kwa ujumla juu ya umuhimu wa elimu na nafasi ya elimu kwenye jamii.

Aliupongeza uongozi wa shule hiyo kwa mchango wao katika ukuaji wa elimu nchini Tanzania.

Mkuu wa Shule hiyo, Laurent Gama, aliipongeza benki hiyo kuwa imekuwa kiungo muhimu katika utekelezaji wa azma ya serikali ya kuongeza ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa elimu bora kwa ngazi zote za elimu nchini.

## Onyo kutumia viuatilifu vya pamba kwenye nafaka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara mkoani Shinyanga, wametakiwa kuacha mara moja kutumia madawa yanayotumika kuua wadudu wanaoshambulia pamba na tumbaku ili kulinda afya ya mtumiaji.

Wakulima wengi wanaolima tumbaku na pamba, wamekuwa wakitumia viwatilifu wadudu vinavyotumia kwenye mazao hayo kwenye mahindi na kusababisha kutengeneza sumbukuvua ambayo ni hatari kiafya kwa mtumiaji.

Ofisa lishe Mtafti, Elimu na Mafunzo lishe Neema Joshua kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe, alitoa onyo hilo wakati wa mafunzo ya umuhimu wa lishe katika kuimarisha kinga dhidi ya magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa kwa wanahabari mkoani wa Shinyanga.

Alisema mkulima anapotumia viwatilifu wadudu vinavyotumia kwenye mazao ya kibiashara na chakula kunasababisha kutengenezwa kwa sumbukuvu ambayo inakwenda kumathiri mtumiaji na mtoto aliyeko tumbani kuwa na udumavu wa akili.

# Mkakati kuongeza uzalishaji korosho

**Na Ashton Balaigwa,** DODOMA

TANZANIA imeanza kujipanga kwa ajili ya kuliteka soko la Afrika la korosho kutokana na uzalishaji bora kuliko nchi nyingi barani na duniani.

Hatua hiyo inatokana na Tanzania kuwa ndio nchi iliyozifundisha kilimo cha korosho nchi za Afrika ikiwamo za Ivory Coast na Nigeria, ambazo kwa sasa zinafanya vizuri na zinaongoza kwa kuzalisha zao hilo Afrika.

Kutokana na hali hiyo sasa Tanzania imeanza mkakati wa kuanza kuongeza uzalishaji wa zao hilo, kwa kuwafundisha wakulima wa zao la korosho katika mikoa 17 ili kuliteka soko hilo.

Mtafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Naliendele kitengo cha Agronomia ya Korosho, Kasiga Ngiha, aliyasema kwenye mafunzo ya wakulima wa korosho kutoka Halmashauri za Kongwa na Mpwapwa mkoani Dodoma.

Alisema takwimu ambazo zimepatikana kutoka mtandao wa kilimo forum.com zinaonyesha kuwa Tanzania ni nchi ya nne kwa nchi za Afrika kwa kuzalisha korosho ikitanguliwa na Nigeria inayoongoza kwa kuzalisha tani za ujazo 900,000 kwa mwaka ikifuatiwa na Ivory Coast inayozalisha tani za ujazo 600,000.

Mtafiti wa magonjwa na visumbufu vya zao la korosho, Dk. Wilson Nene, alisema sababu inayopelekea kuwapo kwa uzalishaji mdogo wa zao hilo nchini ni pamoja na wakulima wamekuwa wakitumia mbegu za kienyeji.

Alisema tayari TARI Naliendele wameanza kuwafundisha wakulima kutumia mbegu bora za kisasa aina 54 zinazozalishwa na TARI Naliendele zenye uwezo wa kuzalisha mti mmoja zaidi ya kilo 20 tofauti na mbegu za kienyeji zinazotoa kilo 11.

Naye Mratibu wa zao la korosho kutoka TARI Naliendele, Dk. Geradina Mzena, alisema wamekuja na mikakati mipya ya kutekeleza agizo la serikali la kuongeza uzalishaji wa zao hilo kutoka tani 315,000 na kufikia tani milioni moja kwa kuwapa wakulima mbinu za kisasa za kilimo hicho pamoja na kutumia mbegu bora za kisasa katika mikoa 17 nchini.



Ofisa Mkuu wa Huduma Shirikishi wa benki ya NMB, Nenyuata Mejooli, akizungumza katika hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na benki hiyo, jijini Arusha juzi, kujadili mikakati ya kuboresha ushirikiano. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CCM yaahidi huduma bora kisiwani

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

WANANCHI wa Kisiwa cha Irugwa kilichopo Ukerewe wameahidiwa kituo cha afya, boti, kivuko na kuboresha huduma za jamii, shule za msingi na sekondari.

Ahadi hiyo ilitolewa na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwenye mkutano wa kampeni akiwaombea kura mgombea urais wa CCM, Dk. John Magufuli, uliofanyika katika Kijiji cha Nabweko kisiwani Irugwa, humo alisema atawajengea kituo cha afya ili wapate huduma karibu na kuwapunguzia umbali wa kusafiri na gharama za kufuata matibabu jijini Mwanza. Alisema pia itanunuliwa boti, kivuko na kuboresha huduma za jamii kwenye sekta ya maji na miundombinu ya shule kutani humo hivyo hawanabudi kuichagua serikali ya CCM iendelee kuleta maendeleo, kutatua changamoto zao na kuwahudumia kwa dhati.

Alisema kuwa kisiwa hicho kina changamoto ya huduma za afya, hivyo baada ya uchaguzi na Rais, wabunge na madiwani kuapishwa kazi ya kwanza ya mbunge wa Ukerewe ni kuhakikisha kituo cha kwanza cha afya Ukerewe kinajengwa Irungwa ili kuwasogezea huduma na kuwaondolea wananchi adha ya kuzifuata jijini Mwanza.

Alisema ukubwa wa Kata ya Irugwa inahitajika kituo cha afya ili wagonjwa wenye matatizo ya kiafya wapate huduma karibu, nje ya hapo ni gharama na watu kupoteza maisha, alidai ujio wake Irugwa mbali na kampeni umelenga kuwajengea kituo cha afya kitakachokuwa karibu na Hospitali ya Bwisya iliyopandishwa hadhi kuwa ya wilaya na itatoa huduma ili kuokoa maisha na kuwapunguzia gharama za kwenda Mwanza na Nansio na yote iko kwenye ilani.

"Nataka niwaambie, tumejenga zahanati 1,498 vijijini na vituo cha afya 498 nchi nzima hapa Ukerewe vitatu (Muriti, Kagunguli na Bwisya kwa zaidi ya Sh. bilioni 1, kitawapunguzia umbali na gharama za kusafiri na kutumia mitumbwi kufuata huduma, baada ya kuapishwa Mkundi aje kuchukua fedha za vituo vya Ukerewe, cha kwanza kujengwa ni Irugwa," alisema Majaliwa.

Nipashe Spotiko




WACHEZAJI 10 WALIOBEBA MATAJI MENGI KARNE 21 UK. 12



## ISIKUPITE

TANGU kuanza kwa msimu uliopita, Manchester United imezawadiwa penalti 20 kwenye Ligi Kuu England (Premier League), idadi ambayo ni kubwa zaidi kuliko ilizozawadiwa timu yoyote kwenye ligi hiyo kwa kipindi hicho.

# MAMBO 10 YA KUVUTIA YA BALE REAL MADRID

**MADRID,** Hispania

KURUDI kwa Gareth Bale kule Tottenham Hotspur kulitawala vyombo vya habari katika wiki ya hivi karibuni, huku raia huyo wa Wales akijiunga na klabu hiyo akitokea Real Madrid kwa mkopo wa muda mrefu.

Akiwa aliondoka pale London Kaskazini kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2013 kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia kwa wakati huo.

Baada ya miaka saba na mataji kadhaa kwa jina lake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, hakuwa na mahusiano mazuri na kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane. Baada ya msimu mgumu wa 2019-20, Bale amerudi Tottenham Hotspur kwa mkopo. Ripoti zinabainisha kwamba Real Madrid na Spurs zimekubaliana kuchangia mshahara wake wa euro 600,000 kwa wiki.

Makala haya yanakuchambulia mambo 10 ya kuvutia ya Bale kwa kipindi alicheza soka lake pale Real Madrid, twende sasa...

### #10. MCHANGO KWA KLABU

Gareth Bale alijiunga na Real Madrid kipindi cha majira ya joto mwaka 2013 na haraka akawa na mchango mkubwa katika klabu. Los Blancos wakati huo ikiwa na wachezaji bora duniani, Cristiano Ronaldo na Karim Benzema wote wakisifiwa kama magwiji wa klabu.

Ni Ronaldo na Benzema pekee ndio wamefunga mabao mengi kuliko Bale kwa kipindi alichokaa pale Santiago Bernabeu, na hilo limethibitisha namna gani raia huyo wa Wales alivyokuwa kwenye ubora wake.

### #9. WASTANI WA BAO KILA MCHEZO ALIOANZA

Kwa wakati huu, Bale ana mabao 105 katika mechi 204 alizoanza kwa Real Madrid, rekodi ambayo imekwenda kuonyesha namna gani raia huyo wa Wales alivyochangia mafanikio ya klabu hiyo kwa hivi karibuni.

Cristiano Ronaldo anaweza kuwa ndiye nembo kubwa kwa klabu hiyo, lakini uwezo wa Bale ulikuwa na mchango mkubwa zaidi kwa miaka michache iliyopita.

### #8. MABAO 556

Kwa pamoja, Bale na Ronaldo wana jumla ya mabao 556 na pasi za mwisho 199, kwa kipindi walichocheza pamoja katika historia ya zama za klabu hiyo.

Bale ana uhakika wa kukumbukwa kama mmoja wa wachezaji bora na waliojitolea kwa Madrid.

### #7. MATAJI MANNE UEFA

Bale alishinda mataji manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pale Real Madrid na alifunga katika fainali mbili za mashindano hayo. Kama ilivyo kwa Ronaldo, yeye pia mara kwa mara alikuwa mchezaji wa mashindano makubwa.

### #6. MATAJI 16

Bale tangu atue Real Madrid ameshinda mataji 16 kwa kipindi chote alichocheza pale. Jumla ya mabao 166 aliyohusika nayo katika mechi 251 alizoicheza klabu hiyo ni moja ya mafanikio makubwa zaidi kwake.

### #5. PASI ZA MWISHO NYINGI KULIKO BECKHAM

Bale licha ya kuonekana kutokuwa na mahusiano mazuri na kocha wake Zidane, lakini takwimu zake haziongopi na ukweli unabaki kwamba atakumbukwa kama mmoja wa wachezaji waliotoa mchango mkubwa zaidi kwa klabu hiyo wakati ikitawala mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ana mataji mengi zaiki kuliko Zinedine Zidane, ana pasi za mwisho nyingi kuliko David Beckham, na ana mabao mengi kuliko gwiji, Ronaldo Nazario. Rekodi ambayo inamfanya kuwa mmoja wa wachezaji muhimu na watakaokumbukwa zaidi klabuni hapo.

### #4. MECHI NYINGI KULIKO FIGO

Amecheza mechi nyingi zaidi kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya kuliko nyota wa zamani wa Real Madrid na mshindi wa Ballon d'Or, Luis Figo, huku pia ameshinda Ligi ya Mabingwa Ulaya mara nyingi zaidi kuliko straika na gwiji, Raul.

### #3. MATAJI YA LIGI MENGI KULIKO SPURS

Akiwa ameshinda mataji mawili ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kwa jila lake kwa kipindi alichocheza kule Hispania, maana yake ni kwamba Bale ameshinda mataji mengi zaidi ya ligi kuliko Tottenham katika historia yao. Atamaliza ukame wa Spurs wa kutoshinda taji la Ligi? Tusubiri.

### #2. MRITHI WA BALE

Wakati Tottenham imejaribu mara kadhaa bila mafanikio kwa miaka ya hivi karibuni kutafuta mrithi wa kuziba pengo la Bale kwa kuwasajili Nacer Chadli, Erik Lamela, na Clinton N'Jie. Lakini sasa kwa kumsajili Bale wamepata mrithi wa Bale ambaye ni Bale mwenyewe.

### #1. REKODI LALIGA

Akiwa na mabao 80 kwa jia lake kwenye Ligi Kuu ya Hispania, hakuna mchezaji yeyote Muingereza aliyewahi kufunga idadi kubwa ya mabao kwenye historia ya LaLiga zaidi ya Bale.

Kwa nyongeza, Bale ni mmoja wa wachezaji saba tu katika historia waliowahi kufunga mabao mawili katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na ni Muingereza pekee kuwahi kufanya hivyo. Alifunga mabao mawili wakati akitokea benchi kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya wakati Real Madrid ikicheza dhidi ya Liverpool mwaka 2018 na kulibeba taji hilo.

Extra Time

# WACHEZAJI 10 WALIOBEBA MATAJI MENGI KARNE YA 21

**LONDON,** England

SOKA la dunia linabadilika kwa kila msimu unaopita, wakati makocha na wachezaji wakiendelea kuonyesha ujuzi wao wa kufikia malengo na mafanikio yao. Hata hivyo, kitu kimoja kimebaki vilevile, kwani katika wote hao kila mmoja anawania kushinda taji, kitu ambacho ndio mafanikio makubwa zaidi katika soka dimbani.

**Watu kama Matt Le Tissier na Antonio di Natale ni wachezaji wa daraja la juu kabisa duniani ambao walistaafu kucheza soka bila kutwaa taji lolote, huku pia kunaweza kuibuka mjadala kwamba, nahodha wa zamani wa Liverpool, Steven Gerrard hakuweza kutwaa mataji mengi katika kipindi chake chote cha uchezaji, wakati pia akilikosa taji la Ligi Kuu ya England.**

Soka la kisasa limetawaliwa zaidi na Real Madrid na Barcelona, huku timu kama Bayern Munich, Juventus, Manchester United, na Liverpool zimekuwa na miaka ya mafanikio ya hivi karibuni.

Kumaliza msimu wakiwa na medali shingoni mwao ni ndoto ya kila mchezaji, huku wakitaka kuongeza mataji mengi zaidi katika kabati zao.

Katika hilo, hapa tunawaangalia wachezaji ambao wameshinda mataji mengi zaidi kwa kipindi chao cha uchezaji cha karne ya 21.

Kumbuka: Takwimu hizi zinafanywa kwenye tovuti ya transfermarkt.com, wakali hao hawa hapa...

### #10 ZLATAN IBRAHIMOVIC | MATAJI 33

Zlatan Ibrahimovic ni mmoja wa mastraika wakubwa zaidi katika kizazi chake na anakwenda kuwa gwiji wa soka la kisasa. Raia huyo wa Sweden amefikia umri wa mwisho na sasa akiwa na miaka 38, na amesaini mkataba wa kudumu na AC Milan hivi karibuni.

Ibrahimovic amezichezea klabu kubwa duniani na kushinda mataji mengi. Yeye ndiye mfungaji wa wakati wote wa Sweden na pia ndiye mchezaji mwenye mafanikio makubwa zaidi nchini humo.

Amezichezea kwa nyakati tofauti, Ajax, Barcelona, Inter Milan, AC Milan, Juventus, Paris Saint-Germain, na Manchester United na Ibrahimovic ameshinda mataji 33 hadi sasa na anaweza kuongeza mengi kabla ya kustaafu.

### #9. SERGIO BUSQUETS | MATAJI 33

Sergio Busquets ni mmoja wa wachezaji wengi wa Barcelona katika orodha hii ambaye amefungana idadi sawa ya mataji na Zlatan Ibrahimovic. Kiungo huyu wa kimataifa wa Hispania, amekuwa na mafanikio makubwa katika kikosi cha Barcelona na timu ya taifa.

Busquets alikuwa chini ya Pep Guardiola pale Barcelona wakati miamba hao wa Calalunya walipolitawala soka la dunia mwishoni kwa miaka ya 2000 na mwanzoni mwa miaka ya 2010. Katika umri wake wa miaka 32, Busquets bado ni mchezaji muhimu kwa klabu na nchini yake akiwa tayari ana mataji 33 mkononi mwake.

### #8. CRISTIANO RONALDO | MATAJI 33

Cristiano Ronaldo kama ilivyo kwa Busquets na Ibrahimovic, ana mataji 33 mkononi mwake na pengine anaweza kuyaongeza katika miaka inayokuja.

Akichukuliwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote, Ronaldo raia wa Ureno amezichezea Sporting CP, Manchester United, Real Madrid na Juventus na pia kwa sasa ni nahodha wa timu ya Taifa ya Ureno.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ameshinda mataji katika ligi mbalimbali, huku akishinda mara tano taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ndiye mfungaji wa wakati wote wa mashindano hayo. Nyota huyo wa zamani wa Real Madrid bado anaendelea kuwa kwenye nafasi kubwa ya kushinda mataji mengi zaidi. Huku akiwa ameshinda Ballon d'Or mara tano, bado anaweza kuongeza mataji kwa miaka inayokuja.

### #7. ARJEN ROBBEN | MATAJI 33

Mchezaji wa nne katika orodha hii aliyeshinda mataji 33, Arjen Robben ambaye kipindi chake cha uchezaji alikuwa mchezaji wa aina yake. Akiwa amechomoza kutoka Groningen, Mholanzi huyu alicheza PSV Eindhoven, kabla ya kwenda kujiunga na Jose Mourinho pale Chelsea.

Baada ya kuondoka Stamford Bridge miaka michache baadaye, akaenda Real Madrid, lakini Robben alikuwa na mafanikio zaidi alipojiunga na Bayern Munich mwaka 2009. Akiwa amebarikiwa kwa uwezo wa kutumia mguu wa kushoto, Robben alitangaza kustaafu soka kipindi cha majira ya joto kilichopita kabla ya kurudi na kujiunga na klabu yake ya utoto ya Groningen.

### #6. HOSSAM ASHOUR | MATAJI 34

Mchezaji pekee ambaye anacheza nje ya Ulaya katika orodha hii ni Hossam Ashour kiungo wa kimataifa wa Misri ambaye kwa sasa anaichezea klabu ya Al Ahly ya nchini kwake. Akiwa ametumia muda wake wote wa uchezaji katika klabu yake hiyo tangu mwaka 2003, Ashour ni mchezaji mkubwa wa klabu hiyo na nchi yake na bado yupo fiti katika umri wake wa miaka 34.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Misri ameichezea klabu hiyo zaidi ya mechi 500 akishinda mataji 34 hadi sasa, huku pia akishinda mataji 12 ya Ligi Kuu akiwa na Al Ahly.

Ashour alianza kuichezea timu ya Taifa ya Misri mwaka 2008 na amecheza jumla ya mechi 14 hadi sasa. Kwa sasa ni nahodha wa Al Ahly na anaonyesha hana mpango wa kutundika daluga hivi karibuni.

### #5. GERARD PIQUE | MATAJI 36

Gerard Pique ni mchezaji mwingine wa Barcelona katika orodha hii, huku Mhispania huyo akitajwa kama mmoja wa walinzi bora zaidi wa kizazi chake. Alijiunga tena na Barcelona akitokea Manchester United mwaka 2008, Pique haraka akawa mchezaji nguzo wa Pep Guardiola na alitengeneza upatina mzuri sana na Carles Puyol.

Kwa timu ya Taifa ya Hispania, Pique ameshinda Kombe la Dunia na lile la Mataifa ya Ulaya kabla ya kustaafu kuichezea La Roya mwaka 2018. Katika umri wake wa miaka 33, mlinzi huyo bado ana nafasi kubwa ya kuweza kutwaa mataji mengine pale Barcelona.

Akiwa na mataji 36 kwa jina lake, Pique ni mmoja wa walinzi bora zaidi wa kizazi chake.

### #4. MAXWELL | MATAJI 37

Maxwell hakuwahi kuwa mchezaji nyota kwa klabu yoyote aliyoichezea, lakini ukweli ni kwamba klabu kubwa duniani zilimtaka mchezaji kama agano kwa uwezo wake na kipaji chake.

Mlinzi huyo wa Brazil alichezea timu kama Ajax, Inter Milan, Barcelona na Paris Saint-Germain na alitengeneza urafiki mkubwa na Zlatan Ibrahimovic.

Maxwell aliichezea mechi saba tu timu ya Taifa ya Brazil na alistaafu soka mwaka 2017 akiwa na mataji 37 kwa jina lake.

### #3. LIONEL MESSI | MATAJI 37

Anatajwa kama mmoja wa wachezaji bora wa wakati wote, Lionel Messi. Alitawala vyombo vya habari katika wiki za hivi karibuni. Baada ya kukaa kwa miongo miwili na Barcelona, nyota huyu wa kimataifa wa Argentina aliamua kutaka kuondoka, kabla ya kubadilisha uamuzi wake.

Katika umri wake wa miaka 33, Messi ameendelea kuwa mchezaji nyota zaidi uwanjani akicheza soka la aina yake. Messi ameweka rekodi ya kutwaa mara sita tuzo ya Ballon d'Or.

Huku akiwa na mataji 37 pale Barcelona, lakini akiwa na wakati mgumu wa kupata mataji na timu yake ya Taifa ya Argentina.

### #2. ANDRES INIESTA | MATAJI 39

Andres Iniesta ni mmoja wa wachezaji waliobarikiwa kuweza kuucheza mchezo huu wa kuvutia. Mhispania huyu alihitimu katika akademi ya kukuza vipaji vya soka pale La Masia na akaja kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa kikosi cha Barcelona kwa miaka mingi.

Akianza kuichezea Barcelona mwaka 2002, akiwa na miaka 16, aliondoka klabuni hapo mwishoni mwa msimu wa 2017-18 na kujiunga na Vissel Kobe ya nchini Japan.

Iniesta mwenye umri wa miaka 36, bado anaichezea Vissel Kobe ya Japan, ambako ameshinda mataji mawili tangu alipojiunga mwaka 2018 na kufikisha 39.

### #1. DANI ALVES | MATAJI 41

Anatajwa kama mlinzi wa kulia bora zaidi wa wakati wote katika kizazi chake, Dani Alves. Raia huyu wa Brazil ana mataji 41 hadi sasa na bado anacheza katika klabu ya nyumbani kwake, akiwa amejiunga na Sao Paulo kutoka Paris Saint-Germain mwaka 2019.

Ni mlinzi mwenye jicho la goli, Alves pia amebarikiwa kasi na uwezo wa kusaidia mashambulizi mara kwa mara.

Alves alichomoza kutoka klabu ya Sevilla na akahamia Barcelona mwaka 2008, ambako alitumia miaka nane kabla ya kwenda Juventus kwa uhamisho huru. Yeye ndiye anayeshikilia rekodi ya kuwa mchezaji mwenye mataji mengi zaidi katika historia ya wacheza soka.



DANI ALVES

## Nukuu

"Kwa uhakika kabisa najivunia kuwa nahodha, lakini si sababu kubwa ya kubaki. Bila shaka ni kazi kubwa kuifanya, lakini haikuwa sehemu ya mimi kubaki hapa. Tangu amekuja hapa [Mikel Arteta], ameleta vitu vingi sana chanya na falsafa mpya kwa upande wetu, nafikiri hilo lilikuwa muhimu na likanifanya kiwango changu kuwa juu na kujihisi kwamba nahitaji kuimarika zaidi. Nafikiri hii ilikuwa sababu kubwa zaidi," **Pierrre-Emerick Aubameyang akitoa sababu ya kusaini mkataba mpya Arsenal.**



"Leo [Leonel Messi] ananijua mimi vizuri na anajua uwezo wangu na kujiamini kwangu. Ni ishara nzuri na fahari kuondoka huku kukiwa na mtazamo chanya nyuma yangu, sasa nimeondoka na kujiunga na kikosi hiki cha ushindani na chenye hamasa kubwa," **Luis Suarez akieleza kujisikia furaha Messi kumlilia wakati akitua Atletico Madrid kutoka Barcelona.**



"Bado tumefungua milango ya kuimarisha timu yetu, tunaangalia machaguo tofauti, ikitegemea na nini kitatokea kwa baadhi ya wachezaji wetu hapa ," **Kocha Mkuu wa Arsenal, Mikel Arteta akieleza nia ya klabu hiyo kuendelea kusajili kabla ya dirisha la usajili kufungwa hapo Oktoba 5, mwaka huu.**






Straika wa Simba, Chris Mugalu, akipongezwa na wenzake baada ya kuifungia timu yake bao la tatu wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Gwambina FC katika Uwanja wa Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**

# REKODI 10 ZAKUVUTIA RAUNDI YA 4 LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

TARATIBU Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2020/21, umeanza kushika kasi, huku msisimuko ukiwa mkubwa kwa mashabiki wa soka nchini, ikiwa imefikia kwenye raundi ya nne sasa.

**Kinachoonekana kuwa Ligi Kuu msimu huu itakuwa ngumu ni jinsi timu zinavyopambana kutafuta ushindi nyumbani na ugenini.**

Timu inayojichanganya inafungwa hata ikiwa nyumbani. Kabla ya mechi za Jumapili tayari kulikuwa na mechi 10 za timu zilizoshinda ugenini, dhidi ya mechi 16 za timu zilizoshinda nyumbani. Ugumu mwingine wa ligi unaonekana pale idadi ya magoli ambayo timu inashinda.

Ni timu chache tu kama Simba, KMC na Polisi Tanzania ndizo zilizoshinda mechi kwa idadi kubwa ya magoli mpaka sasa, lakini zingine zote ni wastani wa bao moja tu, kabla ya mechi za Jumapili. Kwenye makala haya, tunaangalia rekodi mbalimbali zilizowekwa na timu na wachezaji kwenye mechi za raundi ya nne ya Ligi Kuu Bara, shuka nayo...

**1. KMC YAPOTEZA MECHI YA KWANZA**

Hatimaye vinara kwenye raundi tatu za Ligi Kuu, KMC imepoteza mechi yake ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu siku ya Ijumaa, ilipochapwa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

KMC ilishangaza wengi msimu huu ilipoongoza ligi kwa wiki tatu mfululizo, ikishinda pia mechi zote tatu ilizocheza kwa kuichapa Mbeya City mabao 4-0, ikaidungua Prisons 2-1, ikaifunga Mwadui 2-1, kabla ya rekodi yao hiyo safi kutibuliwa na Kagera Sugar kwenye raundi ya nne.

**2. KAGERA SUGAR YAPATA USHINDI WA KWANZA**

Timu ya Kagera Sugar imepata ushindi wake wa kwanza kwenye raundi hiyo, baada ya kuichapa KMC bao 1-0 kwenye uwanja wake wa nyumbani, Kaitaba mjini Bukoba. Bao pekee likifungwa na winga wake hatari, Yusuph Mhilu ambaye alicheza kwa mara ya kwanza akitokea chumba cha majeruhi.

Timu hiyo ilianza kwa kuchapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya JKT Tanzania, ikatoka suluhu bila kufungana dhidi ya Gwambina ugenini na ikafungwa 1-0 nyumbani na Yanga, kabla ya kushinda mechi yake dhidi ya KMC.

**3. AZAM HAIJARUHUSU BAO LOLOTE**

Hadi kufikia raundi ya nne ya Ligi Kuu, timu ya Azam FC ndiyo timu pekee ambayo haijaruhusu bao lolote kwenye wavu wake. Hii ni baada ya Jumamosi kuichapa Prisons ugenini 1-0.

Azam imeonekana kuwa timu yenye ngome ngumu na kipa wao, David Kissu kutoka Gor Mahia amekuwa makini golini, walianza kwa kuichapa Polisi bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza, ikaifunga Coastal Union 2-0, kisha Mbeya City 1-0, kabla ya juzi kushinda 1-0 dhidi ya Prisons.

**4. PRISONS YAPOTEZA NYUMBANI**

Kwa mara ya kwanza timu ya Prisons imepoteza mechi yake ya kwanza nyumbani baada ya kipigo cha bao 1-0 Jumamosi kwenye Uwanja wa Nelson Mandela dhidi ya Azam FC. Kwenye mechi nne ilizocheza, Prisons ilicheza mbili nyumbani, moja ikishinda 1-0 dhidi ya Namungo.

**5. MBEYA CITY YAPOTEZA ZOTE NNE**

Mpaka kufikia raundi ya nne ya Ligi Kuu timu ya Mbeya City imefungwa mechi zote nne, huku ikiwa haijafunga hata bao moja. Ijumaa ilichapwa bao 1-0 dhidi ya Namungo nyumbani na kabla ya hapo ilifungwa mabao 4-0 dhidi ya KMC, ikafungwa tena 1-0 dhidi ya Yanga na pia 1-0 dhidi ya Azam FC.

**6. AZAM YASHINDA ZOTE NNE**

Azam FC ndiyo timu pekee mpaka sasa iliyoshinda mechi zote nne ilizocheza na ushindi kwa asilimia 100. Ilianza kwa kuichapa Polisi bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza, ikaifunga Coastal Union mabao 2-0, Mbeya City 1-0, kabla Jumamosi kushinda 1-0 dhidi ya Prisons.

**7. KAGERA SUGAR NA BAO LAKE LA KWANZA**

Timu ya Kagera Sugar imefunga bao lake la kwanza kwenye raundi ya nne ya Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kutoweza kufanya hivyo kwenye mechi tatu zilizopita. Bao la Yusuh Mhilu Ijumaa iliyopita ikiifunga KMC lilikuwa la kwanza kwa timu hiyo.

Kwenye mechi zilizotangulia ilianza kwa kuchapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya JKT Tanzania, ikatoka suluhu bila kufungana dhidi ya Gwambina ugenini na ikafungwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Yanga.

**8. WAGENI WAANZA TENA KUWA TISHIO**

Wachezaji wa kigeni wameanza tena kuwa tishio kwenye kinyang'anyiro cha kuwania Kiatu cha dhahabu. Tayari Mzibambwe Prince Dube wa Azam anaongoza akiwa na magoli matatu, huku Mnyarwanda Meddie Kagere na Mkongomani Chris Mugalu, Mzambia Cleotus Chama wote wa Simba wakiwa na magoli mawili kila mmoja, pamoja na Mrundi Birigimana Blaise wa Namungo.

**9. GWAMBINA HAIJAZIONA NYAVU MPAKA SASA**

Baada ya kufungwa mabao 3-0 dhidi ya Simba juzi, Gwambina FC wanabaki kuwa timu ambayo haijafunga bao lolote mpaka sasa.

Ilichapwa 1-0 dhidi ya Biashara United, ikatoka suluhu bila kufungana dhidi ya Kagera Sugar, ikachapwa bao 1-0 dhidi ya Ruvu Shooting, kabla ya kukutana na dhahama hilo la Simba.

**10. MUGALU AFUNGA KILA ANAPOINGIA AKITOKEA BENCHI**

Straika mpya wa Simba, Chris Mugalu, ambaye amekuwa akianzia benchi, ameweka rekodi ya kufunga magoli kila anapoingia tena kipindi cha pili zikiwa zimebaki dakika 15 kabla ya kipenga cha mwisho.

Kwenye mechi dhidi ya Biashara United alifanya hivyo akifunga bao la nne, lakini Jumamosi iliyopita alifunga bao la tatu akiwa pia ameingia kipindi cha pili akichukua nafasi ya Kagere.

**JE, WAJUA?**



CHELSEA imeshindwa kumaliza mechi bila kuruhusu bao ('clean sheet') katika mechi 20 kati ya 21 za Ligi Kuu England (Premier League) ilizocheza ugenini ikiwa chini ya kocha Franck Lampard.





# Mapitio sera ya wazee yanukia kukamilika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ipo katika hatua za mwisho kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Wazee ya mwaka 2003, ili kukidhi mahitaji ya sasa.

Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii anayeshughulikia huduma za ustawi na maendeleo kwa wazee, Mwanaisha Moyo, aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua kikao cha kutathmini mradi wa uwajibikaji kwa wazee Tanzania. Mradi huo wa miaka miwili kuanzia mwaka 2018-2020, unasimamiwa na AcT-KPMG(Programu ya uwajibikaji Tanzania), kwa unafadhiliwa na Shirika la Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (DFID) ambapo unatekelezwa na Shirika lisilo la serikali la Helpage International kwenye mikoa 10 ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Kamishna Moyo alisema sera hiyo imepitwa na wakati ambapo mapitio hayo yametokana na tathmini iliyofanywa ya kuangalia utekelezaji, mafanikio na vikwazo vilivyojitokeza wakati wa utekelezaji wa sera hiyo.

"Tumeshaandaa rasmi sera mpya ya wazee na tupo hatua za mwisho kukamilisha ili kuwa na sera mpya itakayozingatia maeneo yote ya msingi yanayolenga kuboresha maisha ya wazee, tunatarajia kabla ya mwaka huu kuisha tutakuwa na sera ya wazee," alisema.

Alisema kuna mambo mengi mapya yamejitokeza na hayakuwa yametamkwa kwenye sera, hivyo itakuwa na maboresho ya kuyatamka na serikali kwa kushirikiana na wadau itafanya ili kuimarisha maisha ya wazee.

Aidha, alisema katika kuhakikisha wazee wanakuwa salama, serikali imeandaa mkakati wa kutokomeza mauaji ya wazee ambao umeanza kutekelezwa 2019 na utaenda hadi 2023 na umetekelezwa kwa kushirikiana na wadau ikiwamo Shirika la Helpage International na kufanikisha kupunguza mauaji hayo kutoka 557 hadi 74.

"Lengo letu ifikapo 2023 mauaji ya wazee yawe historia kwa nchi yetu, pia tumehakikisha tunaboresha afya za wazee kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kule kwenye mamlaka za serikali za mitaa, tuna utaratibu wa kuwatambua na wale wasiojiweza tunawapatia vitambulisho kwa ajili ya matibabu na bima za afya," alisema.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa wazee wasiojiweza kwa sasa serikali inaendesha makazi yao 13 na yamefanyiwa ukarabati mkubwa na wanapata huduma zote za msingi ili wawe na maisha mazuri. Akizungumzia mradi huo wa uwajibikaji, kamishna huyo alitoa rai kwa maofisa ustawi wa jamii kuelimisha jamii juu ya kuwatunza wazee. Kwa upande wake, Mkuu wa Miradi ya Shirika la Helpage International nchini, Leonard Ndamgoba, alisema mradi wa uwajibikaji unaisha mwaka huu na ulikuwa unagusa maeneo matatu ambayo ni kipato kwa wazee, huduma bora za afya na matunzo na kupambana na unyanyasaji na mauaji ya wazee kwa imani za kishirikina.

Alitaja mafanikio yaliyopatikana kupitia mradi huo ni kupunguza mauaji ya wazee, ushiriki wa jamii na serikali katika kuhakikisha wazee wanalindwa.

"Katika afya tumepata mafanikio makubwa ambapo tumetengeneza mkakati wa utoaji huduma bora kwa wazee na tunasubiri uzinduliwe, kwa kuwa huduma nyingi zinazotolewa kwa wazee hazina mkakati zitolewaje, pia kupitia halmashauri kumekuwapo na ongezeko kubwa la wazee wanasema wanapata huduma bora za afya," alisema.



Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, akizungumza kwenye mkutano wa 16 wa wanachama wa Saccos ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wataalamu wa mipango kutengewa bajeti

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dotto James, amesema serikali itatenga bajeti kwa ajili ya wana-mipango ili watekeleze majukumu yao kwa ufanisi ikiwamo kukamilisha miradi ya kimaendeleo inayopatikana kwenye maeneo yao.

James aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akifunga kongamano la wanamipango lililofanyika kwa siku mbili jijini hapa.

Alisema wizara hiyo itaendelea kufanya kazi kwa karibu zaidi na wanamipango ili kutatua kero zinazowakabili.

Aidha, Katibu Mkuu huyo alisema wizara itawasaidia wataalamu hao wa mipango kujiendeleza kitaaluma ili kufanya kazi vizuri za kupanga mipango ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini.

James ambaye ni mlezi wao alisema atahakikisha wizara hiyo inawasaidia kujiendeleza kitaaluma kwa watakaohitaji.

"Nimesikia kuna tatizo la ujuzi, hivyo nitahakikisha wizara inaendeleza kitaaluma ili mfanye kazi kwa kujiamini katika kutekeleza mipango na malengo yaliyowekwa kitaifa," alisema.

Alisema wana-mipango wengi katika halmashauri nyingi nchini wanafanya kazi kwa kukata tamaa na hata wengine wameacha kutekeleza majukumu ya taaluma zao na wamepotea kabisa hawasikiki tena.

"Mimi kama mlezi wenu, sitaruhusu kulea watu ambao wamekata tamaa na hawajiamini, nitahakikisha nawatetea na mnaondokana na hofu ya kutengwa na kutothaminiwa katika maeneo yenu," alisema.

James alisema wataalamu hao watatambuliwa na kuthaminiwa kama kada nyingine wizara itachukua dhamana ya kutatua kero zao zinazohitaji utatuzi wa haraka hasa katika halmashauri.

Aliwapongeza wana-mipango hao kwa kushiriki kikamilifu katika kufanya tathmini na kutoa maoni, michango na mapendekezo ya namna ya kuandaa mpango wa tatu ambao utakuwa bora zaidi kutokana na ushiriki wao hasa uzoefu wa sekta binafsi.

Alisema atasaidiana bega kwa bega na Kimishna wa Mipango ya Kitaifa, Dk. Nicolaus Shombe, kuhakikisha anakuwa na mawasiliano ya karibu na wanamipango hao ili wafanye kazi za ubunifu zaidi kwa kuibua miradi ya maendeleo katika halmashauri zao.

Dk. Shombe alisema, malengo ya kuitisha kongamano hilo yamefikiwa kutokana na mchango mkubwa wa mawazo, maoni na mapendekezo waliyopata kutoka kwa wadau wa mipango.

## Pinda awaomba viongozi wa dini kuombea uchaguzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amewaasa viongozi wa dini nchini kuendelea kuliombea Taifa ili uchaguzi mkuu ufanyike bila kuvuruga amani iliyopo nchini.

Pinda alitoa kauli hiyo juzi jijini hapa wakati akifungua Mkutano wa 16 Chama cha Kuweka na Kukopa (Saccos) cha Ushirika wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Arusha Road.

"Bado kuna haja kwa viongozi wa dini kuombea kampeni iwe na amani na utulivu lakini zifanywe kwa misingi ya kuheshimiana baina ya mgombea na mgombe na kila mmoja katika jamii atambue amani na utulivu ni mambo ya msingi sana," alisema Pinda.

Akizungumzia chama hicho, Pinda aliwataka wanachama wa hao kutumia mikopo kwa ajili ya maendeleo yao na Taifa kwa ujumla na siyo vinginevyo.

"Uwapo wa Saccos nchini umesaidia wananchi kujiongeza na kufanya shughuli za kujiongezea kipato, lakini zimetoa ajira ambapo kutoka mwaka 2015, Saccoss zimeongezeka kutoka 4,206 hadi 6,178 mwaka huu," alisema.

Pia alisema idadi ya wananchi waliojiunga na Saccos mbalimbali nchini imeongezeka katika kipindi hicho kutoka 676,202 hadi kufikia milioni 2.4 huku mitaji, amana, akiba na hisa vikiongezeka kutoka Sh. bilioni 428.8 hadi kufikia Sh. bilioni 819.

Aliwasisitiza wanachama hao kulipa kwa wakati mikopo ili wanachama wote wapate fursa ya kukopa.

Naye Askofu wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, aliwasihi viongozi wa dini kutoegemea upande wowote wa kisiasa.

Mwenyekiti wa Bodi wa Saccos hiyo, Ibrahim Sumbe, alisema chama hicho kilianza mwaka 2004 ikiwa na wanachama 89 ambapo hadi kufikia Agosti mwaka huu kuna wanachama 653.

Alisema ilianza na fedha kiasi cha Sh. bilioni 1.7 ambapo hadi Agosti mwaka huu ina Sh. milioni 600.4.

Alieleza kuwa madhumuni ya kuanzishwa kwake ni kujiinua kiuchumi, ambapo kwa sasa wanatarajia kupanua huduma za kifedha na kujenga mtaji wa uhakika na kuendelea kujiinua kiuchumi.





# Maandalizi ya kampeni za Magufuli Mbeya yakamilika

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, wamesema maandalizi ya kumpokea mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa tiketi ya CCM, Dk. John Magufuli yamekamilika.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mch. Jacob Mwakasole, aliwaambia waandishi wa habari juzi kuwa Dk. Magufuli anatarajiwa kuwasili mkoani humo Septemba 29, mwaka huu, kwa ajili ya kufanya mikutano mbalimbali ya kampeni kwa ajili ya maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28, mwaka huu.

Mwakasole alisema kiongozi huyo atakuwa na ziara ya siku mbili mkoani humo, huku akisema kuwa mkutano mkuu utafanyika Septemba 30, hivyo akawataka wananchi wa maeneo mbalimbali ya mkoa huo kujitokeza kwenda kumpokea.

Alisema Rais Magufuli amefanya mambo mengi na makubwa ya maendeleo mkoani humo, ikiwamo miundombinu ya barabara, afya na elimu, hivyo wananchi wanatakiwa wajitokeze bila kujali itikadi zao za vyama kwenda kumsikiliza kile atakachoahidi.

"Maandalizi yamekamilika na kwa sasa yanaendelea mambo madogo madogo, na tunawaomba wananchi wa mkoa wenye imani tofauti za vyama vyao, waje wasikilize sera za kiongozi wetu huyu ambaye ametufanyia mengi wana-Mbeya," alisema Mwakasole.

Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema kiongozi huyo atapokelewa mchana katika Wilaya ya Mbarali eneo la Igawa, ambapo atafanya mkutano wa barabarani na wananchi kabla ya kuelekea Mbeya Mjini.

Alisema akifika Mbeya Mjini hatafanya mkutano wowote mpaka Septemba 30 asubuhi, ambapo atafanya mkutano kwenye uwanja wa ndege wa zamani uliopo katika Kata ya Iyela jijini hapa.

Alisema kwenye mkutano huo, viongozi wote wa chama kutoka wilaya za mkoa huo, wagombea ubunge na udiwani wote watatakiwa kuwapo kwa ajili ya kiongozi huyo kuwaombea kura kwa wananchi.

Madodi alisema chama hicho kinatarajiwa kupata ushindi wa heshima kwenye ngazi zote kwa maelezo kuwa wananchi wanakikubali na kukiamini tofauti na inavyodaiwa na viongozi wa vyama vya upinzani.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, alisema hali ya usalama katika Mkoa huo iko shwari na kwamba vyombo vyote vya usalama vimeandaliwa kwa ajili ya kulinda mkutano huo.

Alisema tangu shughuli za kampeni zilipoanza kwenye mkoa huo, hakuna vurugu kubwa zilizotokea, na kwamba atahakikisha hali hiyo inaendelea.

"Sisi tupo tayari kuwapokea wagombea wote wa nafasi ya urais kutoka kwenye vyama tofauti na tutahakikisha wanafanya mikutano yao kwa amani na kuondoka wakiwa salama, kwa sasa maandalizi yanafanyika ya kumpokea mgombea wa CCM," alisema Chalamila.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kulinda amani iliyopo kwa kuwaepuka wanasiasa wanaochochea vurugu kwa maelezo kuwa amani iliyopo ndiyo maendeleo ya nchi.

Dk. Magufuli atakuwa mgombea urais wa pili kufanya kampeni katika Mkoa wa Mbeya baada ya mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, kupita mara mbili mkoani hapo.



Ofisa Masoko wa kampuni ya kuuza zana za kilimo ya ETC Agro Tractor, Elia Rajabu (kushoto), akiongoza timu ya wafanyakazi wa kampuni hiyo kujaribu mitambo ya kilimo kwenye moja ya mashamba yaliyopo Rujewa, wilayani Mbarali, juzi, baada ya kuingia makubaliano na Benki ya CRDB kuwakopesha wakulima zana za kilimo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Neema kwa wakulima kukopeshwa zana kilimo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

BENKI ya CRDB imeingia makubaliano na kampuni zinazouza zana mbalimbali za kilimo, kwa ajili ya kuanza kuwakopesha wakulima zana hizo na kulipa kidogo kidogo ili kuimarisha sekta ya kilimo nchini na kukuza uchumi wa wananchi na taifa.

Akizungumza juzi wakati wa kuingia makubaliano na kampuni hizo, Meneja Biashara wa CRDB Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Feruzi Kolongo, alisema mkopo huo hauhitaji dhamana yoyote isipokuwa asilimia atachangia asilimia 25 pekee ya mkopo.

Alisema asilimia inayobakia 75 itachukuliwa na benki hiyo na kwamba lengo la makubaliano hayo ni kuwarahisishia wakulima upatikanaji wa zana hizo na kuinua kilimo biashara nchini tofauti na ambavyo wakulima wengi wanalima kwa mazoea. "Wakulima wetu wamezoea kila wakienda benki kukopa wanatakiwa waweke dhamana ya nyumba, mashamba na mali zingine zisizohamishika, sasa huu mkopo ni tofauti maana dhamana yake ni huo mtambo utakaokopa," alisema Kolongo.

Alisema kwa muda mrefu wakulima walikuwa wanaomba mikopo ya zana za kilimo, lakini ilikuwa vigumu kwa sababu taratibu zilikuwa hazijakaa sawa na kwamba kwa sasa wameweka taratibu vizuri.

Aliwataka wananchi kuchangamkia mkopo huo kwa maelezo kuwa una masharti nafuu na mitambo hiyo itawasaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuongeza kipato pamoja na uhakika wa chakula.

Kwa upande wake mwakilishi wa kampuni zinazouza zana hizo, Elia Rajabu, ambaye ni Ofisa Masoko wa Kampuni ya ETC Agro Tractor, alisema wakulima wengi wasingeweza kununua zana hizo kwa pesa taslimu kutokana na wengi kuwa na uwezo mdogo. Alisema wakulima wengi huwa wanapata pesa kwa msimu hasa baada ya kuvuna na kuuza mazao yao na kwamba wakati mwingine wote huwa wanafanya kazi ya kutumia pesa kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kilimo.

"Huu ubia utasaidia wakulima wetu kupata tija kwenye kilimo, tunaamini kuwa huu ni mkopo sahihi kutokana na aina ya dhamana ambayo inatumika ambayo ni zana yenyewe atakayokopa mkulima," alisema Rajabu.

Baadhi ya wakulima walioshiriki kwenye uzinduzi wa makubaliano hayo, walisema mikopo hiyo imeanza kutolewa kwa muda mwafaka kwa maelezo kuwa miezi hii ndiyo wanayoingia kwenye shughuli za kilimo kwa msimu wa 2020/2021.

Mmoja wa wakulima hao, Amir Mizar, alisema awali matrekta makubwa walikuwa wanatakiwa kulipa Sh. milioni 25, lakini kwa sasa watakuwa wanalipia Sh. milioni 15 ambazo alidai ni rahisi kulipa. Alisema wakulima wengi huwa wanashindwa kupata tija kwenye kilimo kutokana na kutumia zana duni za kilimo yakiwamo majembe ya mkono pamoja na kupanda mazao kwa kutumia mikono badala ya mashine za kisasa.

Mizar alisema kwa sasa kutokana na uwepo wa mikopo hiyo wakulima wengi watahamasika kuingia kwenye kilimo na hivyo kuongeza uzalishaji wa mazao tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

## Sugu, Tulia bado wachuana vikali

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MCHUANO mkali wa ubunge katika Jimbo la Mbeya Mjini kati ya mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Joseph Mbilinyi 'Sugu' na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Tulia Ackson, umeendelea.

Wagombea hao wamekuwa wakipishana kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Mbeya kila mmoja kunadi sera za chama chake, ambapo juzi kila mmoja alivamia ngome ya mwenzake kuwashawishi wananchi wamchaguwe.

Dk. Tulia alivamia Kata ya Ilemi ambayo ni miongoni mwa ngome za CHADEMA tangu Uchaguzi Mkuu wa 2010, ambapo kata hiyo imekuwa ikiongozwa na chama hicho, huku Sugu naye akiwa katika Kata ya Iziwa ambayo haijawahi kuongozwa na upinzani.

Akiwa katika Kata ya Ilemi, Dk. Tulia alipatiwa zawadi ya picha ambayo baadhi ya vijana wamemchora huku wakidai kuwa zawadi hiyo ni ishara kuwa wanamkubali na watampigia kura kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba 28.

Aliwashukuru wananchi hao na kuwahakikishia kuwa endapo watamchagua atahakikisha anawapelekea maendeleo kwenye kata hiyo ikiwamo kuboresha miundombinu ya barabara.

"Mimi ni mama wa connection, nimekuja hapa sio kwa kukurupuka bali nimekuwa nakuja hapa mara nyingi, niliwahi kuja hapa na nilichangia mifuko 100 ya saruji kwa ajili ya Shule ya Msingi Ilemi na nilitoa fedha yangu mfukoni sio za mfuko wa jimbo," alisema Dk. Tulia.

Aliwashukuru vijana wa kata hiyo waliomwandalia zawadi ya picha akidai kuwa zawadi hiyo ni ishara ya ushindi kwake na kwa chama chake cha CCM. Kwa upande wake Sugu aliwataka wananchi waepuke kuhadaiwa na CCM kuwa kitawaletea maendeleo, na kwamba yeye pamoja na CHADEMA ndio suluhisho la matatizo ya nchi.

Alisema kwa muda mrefu Kata ya Iziwa imekuwa ikiongozwa na madiwani wa CCM, lakini hakuna chochote walichowahi kukifanya, na kwamba kata hiyo ina miundombinu mibovu ya barabara.



# Shein aeleza matokeo ya uwekezaji sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali anayoiongoza imeamua kuifanya elimu kuwa ni moja ya vipaumbele vya serikali kwa kuiongeza bajeti ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutoka Sh. bilioni 47.093 mwaka 2010/2011 hadi kufikia Sh. bilioni 178.917 mwaka 2019/2020.

Aliyasema hayo katika hafla maalum aliyoiandaa ya kuonana, kula chakula cha mchana pamoja na kuwakabidhi zawadi wanafunzi waliomaliza masomo ya kidato cha nne mwaka 2019 na kidato cha sita mwaka 2019/2020 na kufaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza katika mitihani yao ya Taifa.

Dk. Shein alisema kuwa kiwango hicho cha bajeti kumeiwezesha Zanzibar kupata mafanikio makubwa ya maendeleo katika sekta ya elimu.

Alisema kuwa dhamira njema ya serikali mipango mizuri iliyowekwa ya kuwekeza kwa kiwango kikubwa katika sekta ya elimu tayari matunda yake yanaonekana kwa kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao ya ngazi mbalimbali.

Alisema lengo la kufikia dhamira ya kutoa elimu bure liliongozwa na Jemedari wa Mapinduzi marehemu Mzee Abeid Amani Karume mwaka 1964 na yeye alipoingia madarakani alifanya kama zilivyofanya awamu zilizotangulia za uongozi kwa kuipa kipaumbele elimu.

Rais Dk. Shein alisema kuwa ufaulu wa wanafunzi katika mitihani yao umeongezeka sana, ambapo wanafunzi wa msingi kwenda sekondari ufaulu umeongezeka kutoka asilimia 84.4 mwaka 2010 na kufikia asilimia 97.5 mwaka 2019.

Alieleza kuwa ufaulu wa wanafunzi kidato cha pili katika mitihani ya kuingia kidato cha tatu umeongezeka kutoka asilimia 58.2 mwaka 2010 na kufikia asilimia 76.8 mwaka 2019.

"Ufaulu wa wanafunzi kwa mitihani ya kidato cha nne kwa daraja la kwanza na pili umeongezeka mara nne zaidi kutoka asilimia 1.5 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 6.3 mwaka 2019," alisema.

Kwa upande wa kidato cha sita, Rais Dk. Shein alisema kuwa ufaulu kwa daraja la kwanza na la pili katika mitihani ya Taifa, kwa mwaka huu wa 2020 umefikia asilimia 33.92 ikilinganishwa na asilimia 7.2 mwaka 2010.

Aidha, aliwapongeza wanafunzi hao waliofanya vizuri wakiwamo wanafunzi 299 wa kidato cha nne na wanafunzi 124 wa kidato cha sita waliopata daraja la kwanza katika mitihani yao ya Taifa iliyopita.

Aliwataka wanafunzi hao kuongeza bidii ili waweze kuifanya vyema zaidi katika masomo yao ya hatua iliyo mbele yao sambamba na kuendelea kuwa na nidhamu na kujiwekea malengo ili waweze kufanikiwa zaidi huko mbele waendako.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Dk. Idris Muslim Hijja, alieleza kuwa wanafunzi wa kidato cha nne wamefanya mtihani wa kumaliza Novemba, 2019 na matokeo kutolewa Januari 2020, ambapo jumla ya wanafunzi 18,647 walifaulu kwa madaraja mbalimbali na 299 wamefaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza.

Alisema jumla ya wanafunzi 2,548 wa kidato cha sita walifanya mtihani wao mwezi wa Juni 2020 na matokeo yao kutoka Agosti 2020, wamefaulu kwa madaraja mbalimbali.

Alisema kuwa kati ya wanafunzi hao 2,548, wanafunzi 124 wamefaulu kwa kiwango cha daraja la kwanza, ambapo katika mwaka huu wa 2020 wanafunzi bora wawili katika ufaulu wa masomo ya biashara kwa Tanzania.




Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Balozi Mohamed Ramia Abdiwawa (kulia), akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuzindua tawi jipya la benki ya NCBA Tanzania Ltd, katika Mtaa wa Mlandege, jijini Zanzibar juzi. Wa (pili kulia) ni Mkurugenzi Mkuu wa Benki hiyo, Margaret Karume. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wafamasia wakumbushwa maadili

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Abdullah Mzee, amewataka wafamasia kufuata maadili ya kazi zao ili kulinda heshima katika kada yao.

Aliyaeleza hayo katika hotuba yake ya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wafamasia Duniani iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara Mjini Zanzibar.

Alisema wafamasia ni moja kati ya kada muhimu katika sekta ya afya ambayo inahitaji watendaji waaminifu na wenye uadilifu katika kutekeleza kazi zao.

Alisema wafamasia wanamchango mkubwa katika jamii ikiwamo kutoa elimu ya matumizi sahihi ya dawa katika kukinga na kutibu maradhi.

Alieleza kuwa wafamasia wana wajibu wa kuhakikisha usalama wa dawa kwa wagonjwa wakati wa usambazaji hadi kumfikia mtumiaji.

Kutokana na umuhimu wa kada ya afya, aliwataka wafamasia, madaktari, wauguzi na wataalamu wa kada hiyo kushirikiana ili kulinda afya za wananchi.

Aidha, aliwashauri wafamasia kufikiria njia bora ya kuziendeleza dawa za asili ili kupiga hatua za kimaendeleo kama zilivyo nchi nyingine zikiwamo India na China.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wafamasia Zanzibar, Mohammed Kheir, aliwasisitiza wafamasia kushirikiana na kuwa waangalifu katika kutekeleza majukumu yao ili kutoa huduma bora kwa wananchi.

# Mwinyi awaonya vijana kutumika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Ulinzi na Jeshi la kujenga Taifa wa Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amewataka vijana kutokubali kuyumbishwa na kutumiwa na watu kwa kisingizio cha kisiasa au dini.

Alisema uvunjifu wa amani unapotokea chanzo chake ni vijana kutokana na kutumiwa na watu ambao hawana nia njema na nchi yao.

Aliyasema hayo katika kongamano la siku ya amani duniani lililofanyika Mjini Zanzibar.

Alisema watu wengi hudhani amani inaletwa na vyombo vya ulinzi na usalama bali amani huletwa na utulivu wa wananchi na kupata maendeleo.

"Sio idadi ya askari tulionao, ubora wa zana za kijeshi tulizonazo zinazoweza kuleta amani bali amani huletwa na utulivu wa wananchi na Tanzania tunajivunia kuwa na wananchi wapenda amani," alisema.

Dk. Mwinyi ambaye ni mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), alisema jukumu la kila mmoja ni kuhakikisha kwamba amani tuliyonayo inaendelea kudumu.

Alieleza kuwa zipo nchi ambazo zimeichezea amani na kupelekea machafuko zikiwamo Syria, Yemen, Iraq, DRC na zingine.

"Nchi hizi ziwe fundisho tosha kwetu kuona athari za kuivuruga amani...ni hatari kubwa hasa kwa wanawake na watoto, Tanzania tunahitaji amani katika kuwaletea maendeleo wananchi wetu, hivyo sisi tuwe ni sehemu ya kuijenga na kuiendeleza amani yetu," alisisitiza.

Naye Katibu Mtendaji wa Baraza la Vijana Zanzibar, Khamis Faraj Abdalla, akitoa salamu za vijana, alisema siku hiyo ina lengo la kuimarisha umoja na mshikamano wa taifa lao sambamba na kuwapa elimu ya uzalendo katika kulinda amani ya nchi wakati wote.

Akizungumzia lengo la kuunda mabaraza ya vijana, alisema ni kuwaunganisha vijana pamoja na kuwajenga kuwa wazalendo katika kuitetea nchi yao.

# Maofisa utumishi wanolewa mfumo mpya taarifa

**Na James Mwanamyoto,** DODOMA

MAOFISA utumishi na maofisa tawala 108 waliohitimu mafunzo ya siku 12 ya mfumo mpya wa kitanzania wa taarifa za kiutumishi na mishahara, wametakiwa kukamilisha usahihishaji wa taarifa za watumishi kwenye mfumo wa sasa, ili ziweze kuingizwa katika mfumo mpya.

Maelekezo hayo yametolewa jana jijini hapa na Kaimu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Cosmas Ngangaji, wakati akifunga mafunzo hayo yaliyokuwa na lengo la kuboresha utendaji kazi na usimamizi wa rasilimaliwatu na mishahara.

Ngangaji alisema, baada ya kukamilika kwa mafunzo hayo, serikali inatarajia mfumo mpya utatumika kutatua kero za watumishi kwa ufanisi na kwa haraka zaidi ikiwa ni pamoja na kuwaondolea usumbufu wa kufuata huduma Ofisi ya Rais Utumishi.

Alisema, mfumo mpya utaongeza uadilifu kiutendaji kwa kuwa umewezeshwa kurekodi matukio yote yatakayokuwa yakifanywa na maofisa waliopewa dhamana ya kutumia mfumo huo.

"Serikali kupitia mfumo huu itakuwa ikifuatilia na kujua ni ofisa yupi amefanya nini au amekusudia kufanya nini, wapi na muda gani," alifafanua.

Alisema mfumo mpya utaimarisha uwajibikaji na kuwawezesha watumishi kufuatilia utekelezaji wa masuala mbalimbali ya kiutumishi yanayowahusu kupitia simu na barua pepe hivyo, kuongeza uwajibikaji na kujiepusha kufanya kazi kwa mazoea.

"Watumishi wa umma watakuwa wakipata taarifa na kujua kama kazi iliyofanyika bado ipo kwa Ofisa Utumishi, Mwajiri au imeshatumwa utumishi kwa ajili ya kuidhinishwa," alisisitiza.

Naye Mkuu wa Idara ya Utawala, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, Martin Ndilanha, kwa niaba ya washiriki wa mafunzo amemhakikisha Ngangaji kuwa, wamepata mafunzo bora ya mfumo mpya na kuwa wabobezi katika kuutumia ili kuondoa kero na changamoto zilizokuwa zikiwakabili watumishi wa umma nchini.

Ndilanha alisema, mfumo huo mpya ulioboreshwa unapunguza uzalishaji wa madeni kwa serikali, unarahisisha na kupunguza gharama za uandaji wa bajeti ya serikali na kwamba wako tayari kuutumia ipasavyo.

Serikali imepanga kuanza matumizi rasmi ya mfumo huu mpya mwezi Novemba, 2020 baada ya kukamilisha mafunzo kwa makundi manne ya maofisa utumishi na maofisa tawala mwishoni mwa mwezi Oktoba, 2020.




Wadau wa sekta ya madini na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki (kulia), wakisikiliza maelezo kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wateja Binafsi wa benki ya NBC, Elibariki Masuke (katikati), wakati waziri huyo, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maonyesho ya madini mkoani Geita. Wengine ni Waziri wa Madini, Dotto Biteko (wa tatu kushoto) na Meneja Uhusiano na Serikali wa benki hiyo, William Kallaghe (kushoto). **MPIGAPICHA WETU**

# Washukuru kuchangiwa mil. 5/- ujenzi wa shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Nyihogo Halmashauri ya Mji wa Kahama mkoani Shinyanga, wamempongeza mgombea urais kwa tiketi ya CCM, Rais John Magufuli kwa kuwachangia Sh. milioni tano za ujenzi wa Shule ya Msingi Mayila.

Walisema kuwa fedha hizo zimesaidia kukamilisha ujenzi wa shule hiyo ambayo imejengwa kwa nguvu za wananchi.

Walisema, lengo la ujenzi wa shule hiyo ilikuwa kuwanusuru wanafunzi wasiendelee kugongwa na magari ya mizigo wakati wa kuvuta barabara inayokwenda nchi za jirani za Rwanda, Uganda, Burundi na DRC Kongo, kwenda Shule ya Msingi Kilimo.

Wananachi hao walitoa pongezi hizo jana wakati wa ufunguzi wa kampeni Kata ya Nyihogo, Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Kata hiyo imegawanyika sehemu mbili baada ya kupita katikati mwa barabara inayokwenda nchi za jirani na kulazimika baadhi ya wanafunzi wa upande mmoja kuvuka barabara.

Shedrack Nkwami, diwani aliyemaliza muda wake alisema kuwa, kabla ya kujengwa kwa shule ya Mayila, wanafunzi wa kata hiyo hasa wa awali waligongwa na magari ya mizigo na kusababisha vifo vyao.

Vile vile, alisema kutokana na vifo vya wanafunzi mara kwa mara, alichukua jukumu la kuwahamasisha wananchi na kujenga Shule ya Mayila ambayo ilichangiwa Sh. milioni tano na Rais Magufuli, kuwanusuru watoto.

Mwananchi Julieth Joseph, alisema anampongeza mgombea urais wa CCM kwa kutoa mchango ambao ulikamilisha ujenzi wa shule hiyo na sasa wanafunzi wanaendelea na masomo na hakuna tena vifo vinavyojitokeza kwasababu ya kugongwa na magari makubwa.

Mgombea udiwani wa kata hiyo, William Singano alisema, ataanza kutekeleza maendeleo pale alipoishia diwani aliyemaliza muda wake na kuongeza katika eneo ilipojengwa shule hiyo kunazaidi ya hekari 12 atahakikisha kunajengwa shule ya sekondari ili kuendelea kusogeza elimu karibu.

# Maonyesho ya madini yatajwa kuwa na tija

**Na Mwandishi Wetu**

MAONYESHO ya madini na teknolojia yaliyomalizika jana mkoani Geita, yametajwa kuwa na tija kubwa kwa wadau wa sekta ya madini na serikali.

Hayo yameelezwa na Benki ya NBC ambayo ilikuwa miongoni mwa taasisi zilizoratibu maonyesho hayo, na kueleza mkakati wake wa kutekeleza kwa vitendo masuala muhimu iliyoahidi kuyafanya kwa kushirikiana na wadau hao ili kuboresha zaidi sekta hiyo.

Akitoa tathmini ya ushiriki wake katika maonyesho hayo yaliyofungwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, aliyemwakilisha Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Mkurugenzi wa Idara ya wateja binafsi wa benki hiyo, Makao Makuu, Elibariki Masuke, alisema katika kipindi chote cha maonyesho hayo, benki hiyo ilifanikiwa kuendesha programu mbalimbali ikiwamo mafunzo kwa wadau takribani 600 wa sekta ya madini wakiwamo wachimbaji wadogo na wajasiriamali.

"Pia mbali na huduma za kibenki ikiwamo kufungua akaunti mpya kwa wateja, tumefanikiwa kuendesha kliniki za biashara ambapo tuliweza kuwakutanisha wafanyabiashara na taasisi au mamlaka mbalimbali zinazogusa biashara zao. Zaidi, kupitia makongamano mbalimbali tumewawezesha wadau wa sekta ya madini kubadilishana mawazo baina yao wenyewe, lakini baina yao na mamlaka mbalimbali za serikali ikiwamo Wizara ya Madini, TRA, NEMC, SIDO na TANTRADE, TABWA, OSHA, GST na NSSF," alisema.

Aliongeza kuwa ili kuhakikisha mafunzo yaliyotolewa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na wadau wengine yanaleta tija iliyokusudiwa kwa wadau wa sekta ya madini, benki hiyo inaandaa mkakati wa utekelezaji wa masuala muhimu yaliyoafikiwa ikiwamo kuja na huduma maalum ya kibenki mahususi kwa ajili ya wadau wa sekta ya madini.

Kwa upande wake Meneja Uhusiano na Serikali wa Benki hiyo, William Kallaghe, alisema kupitia maonyesho haya benki hiyo imeweza kujadiliana na serikali pamoja na kampuni kubwa ikiwamo migodi mikubwa ambapo kwa pamoja wameona umuhimu wa kampuni hizo kutoa mikataba ya kisheria kwa wazabuni wao, ili kupitia huduma ya mikopo isiyo na dhamana inayotolewa na benki hiyo iweze kuitumia mikataba hiyo kuwakopesha zaidi wazabuni hao.

Kufuatia maelezo hayo Waziri Kairuki aliiagiza benki hiyo kuhakikisha inawasilisha maoni yote ya wadau wa sekta ya sekta madini yaliyokusanywa kupitia Kliniki ya Biashara ya benki hiyo na iyawasilishe kwenye ofisi yake kwa kushirikiana na Wizara ya Madini ili yaweze kufanyika kazi.

## Mapigano yazuka mpakani mwa Syria

**BEIRUT,** Lebanon

KUMETOKEA mapigano makali kati ya vikosi vya usalama vya Lebanon na makundi ya wanamgambo wa Kiislam wenye itikadi kali, kaskazini mwa Lebanon, karibu na mpaka wa Syria, mwishoni mwa wiki.

Mapigano hayo yamesababisha vifo kadhaa katika kambi zenye silaha na wapiganaji wengi kujeruhiwa kwa mujibu wa vyanzo vya usalama.

Mapigano hayo yalizuka wakati maofisa polisi wakiwa kwenye operesheni kijiji kimoja, Kaskazini mwa Lebanon, kusaka makundi ya wanamgambo wa Kiislam wanaoshukiwa kupanga mashambulizi.

Watuhumiwa hao, karibu 15, waliweka upinzani mkali, wakitumia silaha za kivita na mabomu.

Vikosi vya usalama vilijibu kwa silaha kubwa na zile za kurusha mabomo, milipuko ambayo ilisikika sehemu nyingi kaskazini mwa nchi hiyo.

Septemba 14, mwaka huu, wanajeshi wanne waliuawa wakati wa operesheni ya jeshi, Kaskazini mwa Lebanon, nyumbani kwa mwanajihadi,

Khaled el-Tellaoui, ambaye alipigwa risasi siku hiyo, alihusishwa katika mauaji ya watu watatu, pamoja na maofisa wawili wa polisi wa manispaa, katika kijiji kimoja Kaskazini mwa LIbanon, Agosti 22. **RFI**

## Korea Kaskazini yaishtukia Kusini shughuli za kijeshi

**PYONGYANG,** Korea Kaskazini

KOREA Kaskazini imesema ilikuwa inautafuta mwili wa raia wa Korea Kusini, aliyeuawa na wanajeshi wake, lakini ikionya kwamba shughuli za kijeshi zinazofanywa na Korea Kusini zinatishia kuongezeka kwa wasiwasi.

Kulingana na Shirika la Habari la Korea Kaskazini (KNCA), limesema mamlaka za nchini humo, zilikuwa zinazingatia namna ya kuukabidhi mwili huo kwa Korea Kusini, iwapo utapatikana.

Ripoti ya KNCA ililiita tukio hilo kuwa ni baya na ambalo halikutakiwa kutokea, ingawa ilionya kwamba shughuli za kijeshi za Korea Kusini karibu na eneo kulikotokea tukio hilo, zilikuwa zimevuka na kuingia kwenye eneo la maji ya Korea Kaskazini na kutaka kusimamishwa kwa shughuli hizo ili kuepusha hali ya wasiwasi.

Msemaji wa Wizara ya Ulinzi ya Korea Kusini, alipoulizwa alisema hawezi kuzungumzia tuhuma hizo za Korea Kaskazini, kwa sasa. **DW**

# Texas yatoa tahadhari maji ya mfereji yanayokula ubongo

**TEXAS,** Marekani

WAKAZI wa Mto Jackson, Texas, nchini Marekani, wameombwa kutotumia maji ya mfereji kwa hofu kuwa huenda yameathirika kwa kijidudu kinachokula ubongo.

Mamlaka ya maji ya eneo hilo, imeonya kwamba kuna uwezekano maji yanayotumiwa na wenyeji, wakazi takribani 27,000 yameingia kijidudu kwa jina Naegleria fowleri.

Kijidudu hicho kawaida huathiri watu, iwapo maji yaliyoathirika yataingia mwilini kupitia puani, na husababisha kifo.

Walioathirika kwa kijidudu hicho, dalili ni pamoja na kiwango cha juu cha joto, kuhisi kichefuchefu, kutapika pamoja na shingo kukakamaa na kichwa kuuma na idadi kubwa walioathirika hufariki dunia ndani ya wiki moja.

**Jamii nane huko Texas, ziliarifiwa Ijumaa usiku, kutotumia maji ya mfereji, kwa matumizi yoyote yale isipokuwa tu kwa kusafisha choo.**

Maambukizi ni nadra sana kutokea nchini Marekani huku visa 34, vikithibitishwa kuripotiwa kati ya mwaka 2009 na 2018.

Jamii nane huko Texas, ziliarifiwa Ijumaa usiku, kutotumia maji ya mfereji, kwa matumizi yoyote yale isipokuwa tu kwa kusafisha choo.

Tahadhari hiyo iliondolewa Jumamosi kwa kila mmoja, isipokuwa kwa wanaoishi karibu na mto Jackson. Tume ya Mazingira huko Texas ilisema "wakazi wa mto Jackson wasitumie maji ya mfereji hadi mfumo wa maji utakaposafishwa vizuri na pia vipimo vionyeshe kwamba maji hayo ni salama kwa matumizi".

Tume hiyo ilisema kwamba bado haijafahamika mchakato huo utachukua muda gani.

Kijidudu cha Naegleria fowleri kinapatikana karibu kote duniani.

Kituo cha Udhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) kilisema maambukizi mengi Marekani, yamesababishwa na majisafi yaliyoathirika katika majimbo ya kusini.

CDC, kilisema watu hawawezi kupata maambukizi kwa kunywa maji yaliyoathirika kwa kijidudu hicho na pia hakiwezi kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine.

Mji wa Florida nchini Marekani, pia uliathirika na maambukizi ya aina hiyo, mapema mwaka huu.

Wakati huo, maofisa wa afya huko walisihi wenyeji kuhakikisha maji ya mfereji pamoja na vyanzo vingine hayapiti kwa njia ya pua. **BBC**



Polisi wakielekea kwenye eneo la kutoa heshima kwa ofisa mwenzao, Matt Ratana, aliyeuawa kwa risasi akiwa kazini katika kituo cha Croydon, jijini London hivi karibuni. **PICHA: BBC**

# 'Lukashenko lazima aondoke'

**PARIS,** Ufaransa

RAIS wa Ufaransa, Emmanuel Macron, amesema katika mahojiano na Gazeti la Le Journal du dimanche, kwamba Rais wa Belarus, Alexander Lukashneko, 'anapaswa kuachia ngazi.'

"Kinachoendelea Belarus ni mgogoro wa kiutawala, utawala wa kimabavu ambao hauwezi kukubali mtazamo wa kidemokrasia na ambao uko kwa kutumia nguvu.

"Ni wazi kwamba Lukashenko lazima aondoke", alisema rais wa Ufaransa, ambaye amenukuliwa na gazeti hilo.

Rais wa Macron, pia alisema "anavutiwa na ujasiri wa waandamanaji" nchini Belarus. Wanajua hatari wanazochukua kwa kuandamana kila mwishoni mwa wiki na bado wanaendelea na maandamano ya kutaka kukomaza demokrasia katika nchi hii ambayo demokrasia imeminywa kwa muda mrefu."

Alisema wanawake hasa, ambao wanaandamana kila Jumamosi, wanastahili kupewa heshima kubwa.

Zaidi ya watu 90, wengi wao wakiwa wanawake, walikamatwa Jumamosi wakati wa mikusanyiko ya upinzani, shirika moja lisilo la kiserikali, lilisema.

Kuhusu jukumu la Rais wa Urusi Vladimir Putin katika kutafuta suluhu ya mzozo wa kisiasa baada ya uchaguzi wa Rais Lukashenko, Agosti 9, unaoendelea kupingwa, Macron alisema kuwa jitihada hizo za Putin bado ni ndoto.

Macron atafanya ziara yake ya kwanza Lithuania na Latvia kuanzia leo hadi Jumatano, nchi mbili za Baltic ambazo ana imani kuwa zitasaidia katika mgogoro huo wa kisiasa nchini Belarus na shinikizo la Urusi. **RFI**

## Washinikiza Netanyahu kujiuzulu

**JERUSALEM,** Israel

MAELFU ya Waisrael walikusanyika nje ya makazi rasmi ya Waziri Mkuu, Benjamin Netanyahu, juzi, wakitaka waziri huyo kuachia ngazi, huku wakiongeza mbinyo dhidi ya kiongozi huyo baada ya wiki kadhaa za maandamano, licha ya hatua za hivi karibuni za kufunga shughuli.

Israel ilirejesha hatua kali za kufunga shughuli kuanzia Ijumaa iliyopita, wakati ikipambana na mlipuko mbaya kabisa wa virusi vya corona ambazo ni pamoja na kufunga baadhi ya biashara, kuzuia mikusanyiko mikubwa na kuwataka watu kubaki nyumbani.

Lakini wabunge wa Knesset hawakukubaliana na mapendekezo ya sheria hiyo ambayo imekuwa ikishinikizwa na Netanyahu, wakisema inalenga kuzuia haki za waandamanaji.

Netanyahu, ambaye amekuwa mamlakani tangu mwaka 2009, ametishia kutangaza hali ya dharura ili kuhitimisha machafuko hayo. **DW**

# GUARDIOLA ALALAMIKIA UGUMU RATIBA ENGLAND



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amelaumu mamlaka ya soka kwa kushindwa kufanya kazi yao ipasavyo kutokana na ratiba ngumu, akisisitiza wachezaji "si mashine".

Mechi zimekuwa zikipangwa kwa mfululizo baada ya msimu kuvurugwa na mlipuko wa virusi vya corona, huku City jana Jumapili ilikuwa inacheza na Leicester City kwenye mchezo wa Ligi Kuu, baada ya kutoka kupata ushindi Alhamisi katika mchezo wa EFL.

City haina wachezaji kama Gabriel Jesus kutokana na kuwa majeruhi ambapo pia wanawakosa Sergio Aguero, Bernardo Silva, Joao Cancelo na Oleksandr Zinchenko.

Guardiola na City walipewa wiki ya ziada kabla ya ufunguzi wa msimu ambapo waliibuka na ushindi katika mchezo wa kwanza dhidi ya Wolves wakitoka kutolewa kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Guardiola aliwaambia waandishi wa habari: "Hakuna anayejali kuhusu wachezaji. Ni suala la biashara. Lakini ukweli hauko hivyo.

"Si tu kwa Man City, ni kwa klabu zote za nchini. Hakuna anayejali kuhusu wachezaji.

"Kila mmoja - Ligi Kuu, UEFA, EFL - wote wanaangalia biashara zao kwanza na si nafasi ya wachezaji.

"Wachezaji walikuwa na wiki mbili tu za maandalizi ya msimu mpya na sasa unatakiwa kucheza kila baada ya siku tatu kwa miezi 11."

# Zidane asherehekea ushindi wa 100 LaLiga

**MADRID,** Hispania

ZINEDINE Zidane alipata ushindi wake wa 100 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, kama Kocha Mkuu wa wa Real Madrid, Jumamosi.

Zidane alifikisha mechi hizo ambazo ni sawa na karne moja wakati Madrid ikiibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Real Betis iliyomaliza na wachezaji 10 uwanjani.

Gwiji huyo wa Ufaransa, ambaye alisherehekea taji lake la pili la LaLiga akiwa kocha wa Madrid msimu uliopita, ameiongoza katika mechi 147.

Zidane anashika nafasi ya pili kwa kocha aliyeshinda mechi nyingi za ligi katika historia ya Madrid, nyuma ya Miguel Munoz mwenye mechi za ushindi 257.

Katika awamu yake ya pili kwenye ukocha pale Santiago Bernabeu, Zidane ambaye ushindi wake wa kwanza aliupata Januari 2016, ameshuhudia timu yake ikifunga mabao 342 huku ikiruhusu 142.

Madrid huo ulikuwa ushindi wake wa kwanza kwa msimu huu wa 2020-21, baada ya wiki iliyopita kutoka sare dhidi ya Real Sociedad.

Baada ya Federico Valverde kufungua pazia la magoli dakika ya 14 kwa Madrid, Betis ilijibu kwa kasi mashambulizi kwa kufunga mabao mawili ndani ya dakika tatu, kupitia Aissa Mandi na William Carvalho.

Emerson ambaye anamilikiwa na Barcelona alijifunga dakika tatu baada ya kipindi cha pili kabla ya kutolewa nje zikiwa zimesalia dakika 23 na Madrid wakapata ushindi kwa bao la penalti ya Sergio Ramos dakika ya 82.





# *Conte ataka Inter kuimarika zaidi*

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte alifurahia mabadiliko yake kulipa wakati Inter ikiibuka na ushindi wa 4-3 dhidi ya Fiorentina kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, lakini ameonya bado wanahitaji kuimarika zaidi.

Inter ilitoka nyuma kwa mabao mawili ndani ya dakika tano za mwisho na kupata ushindi huo kwenye mchezo wa ufunguzi wa ligi dhidi ya Fiorentina katika dimba la San Siro.

Franck Ribery alikuwa kwenye kwango cha kuvutia kwa Fiorentina na alifunga mabao mawili kipindi cha pili.

Ribery alitolewa nje dakika ya 83, huku Fiorentina wakimpa nafasi ya kupumzika, lakini wakajikuta wakifungwa mabao ya dakika za majeruhi kutoka kwa Romelu Lukaku na Danilo D'Ambrosio na kuwapa Inter pointi zote tatu.

Kocha wa Inter, Conte aliwaingiza Achraf Hakimi na Alexis Sanchez, na ndio waliochangia kwa kiasi kikubwa kupatikana kwa mabao hayo ya dakika za majeruhi.

Kama ilivyokuwa kwa Hakimi, mchezaji wa zamani wa Barcelona, Arturo Vidal alikuwa benchi na aliichezea Nerazzurri kwa mara ya kwanza kipindi cha pili.

Baada ya mchezo huo, Conte aliiambia tovuti ya klabu hiyo: "Mabadiliko yalileta manufaa. Nina furaha na vijana wangu wanajua hilo. Utakuwa msimu mrefu na wa kuchosha. Kuna nafasi kwa kila mmoja na kila mtu atahitajika.

"Pointi tatu ni muhimu, tulikuwa na nafasi nyingi na tulitumia nafasi nne kwa kufunga mabao."




# HANSI FLICK SASA ATAKA KAZI BAYERN

**MUNICH,** Ujerumani

HANSI Flick hatakubali kuchoka iwe sababu ya Bayern Munich kufanya vibaya msimu huu kutokana na ratiba kuwabana.

Mabingwa hao wa Bundesliga waliongeza taji la nne chini ya Flick Alhamisi iliyopita wakati walipowafunga Sevilla 2-1 katika muda wa ziada kwenye mchezo wa Super Cup, kule Budapest, Hungary.

Na jana Jumapili Bayern ilianza mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya Ujerumani kwa kucheza ugenini dhidi ya Hoffenheim.

Flick anaelewa kwamba, Bayern imecheza chini ya saa 72 ikitoka kuivaa Sevilla na hivyo hatarajii kuona timu hiyo ikifanya vibaya kwa sababu ya kuchoka.

"Tunatakiwa kuona namna gani kila mmoja akiwa pamoja," alisema Flick.

"Hatutakiwi kutumia sababu ya kuchoka na kufanya vibaya kwenye ligi. Tunatakiwa kupambana kwa nguvu zote."

## Koeman: Mimi si mtu mbaya kwa Suarez

**BARCELONA,** Hispania

RONALD Koeman amesisitiza hakuwa "mtu mbaya" kwa Luis Suarez kuondoka Barcelona, ingawa anaweza kuelewa hasira ya Lionel Messi kuhusu uhamisho huo.

Suarez, anashika nafasi ya tatu kama mfungaji bora wa wakati wote wa Barcelona, aliondoka pale Camp Nou katikati ya wiki na kwenda kujiunga na Atletico Madrid.

Iliripotiwa kwamba, Suarez alikuwa mmoja wa wachezaji wakubwa nyota walioarifiwa na kocha mpya, Koeman kuondoka klabuni hapo baada ya msimu mbaya wa 2019-20.

Lakini Koeman alibainisha hakuwa na nia mbaya naye na kwamba, Suarez angeweza kubaki, lakini hangepata nafasi kubwa ya kucheza.

"Inaonekana kama nilikuwa mtu mbaya kwenye uhamisho huu, lakini si hivyo," alisema Koeman kuelekea mchezo wa kwanza wa Blaugrana hao kwenye LaLiga dhidi ya Villarreal.

"Tangu nilipozungumza kuhusu majaliwa ya Suarez, nimeonyesha heshima kubwa kwake na mara zote nilimwambia itakuwa ngumu kwake kucheza, lakini kama angebaki angekuwa kwenye kikosi chetu.

"Kabla ya kusaini mkataba mpya, klabu ilikuwa inafikiri kuhusu vitu vingi, na nimejaribu kutoa sapoti kwa vitu vyote hivyo. Si tu maamuzi ya kocha."





## Lampard akataa kumlaumu Silva

**LONDON,** England

FRANK Lampard hakuwa na mpango wa kulaumu matokeo ya mchezo baada ya makosa kutoka kwa Thiago Silva katika mchezo wake wa kwanza wa Ligi Kuu ya England na alisema mlinzi huyo wa kati wa Brazil atakuwa muhimu kwa Chelsea.

Makosa ya Silva yalichangia West Brom kupata mabao matatu ya kupindi cha kwanza pale kwenye dimba la The Hawthorns, wakati Blues hao wakilazimika kupigana na kupata sare ya 3-3, shukrani kwa mabao ya Mason Mount, Callum Hudson-Odoi na Tammy Abraham.

Ulikuwa mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu ya England kwa mlinzi huyo mkongwe akiwa na umri wa miaka 36 na bahati mbaya mambo yalionekana kuwa mabaya kwa upande wake.


Kocha wa Chelsea, Lampard alisema Silva ni mchezaji mwenye uzoefu wa kutosha na ana uwezo wa kurekebisha makosa yake mwenyewe bila kuhitaji kuambiwa.

"Sikilizeni, Thiago Silva atakuwa mchezaji muhimu sana kwetu sisi, amefanya mengi katika kipindi chake cha uchezaji," alisema Lampard akiwaambia waandishi wa habari baada ya mchezo huo.

"SitamWangalia yeye, naweza kuzungumza kuhusu makosa kwani yapo wazi - yapo wazi na tunatakiwa kuzungumza kwa uwazi kuhusu hilo, lakini siwezi kumlaumu.

"Sisi ni timu ambayo tuliweza kujibu haraka mashambulizi yake na bahati nzuri tukapata sare."

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# SOLSKJAER AMCHAMBUA POGBA, ASEMA BADO

Amekosa mambo mengi wakati wa maandalizi ya msimu mpya kwa sababu alikuwa mgonjwa, hivyo...

**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesema Paul Pogba bado hayupo fiti kamili, lakini kiungo huyo wa Manchester United "ubora wake unakuja" baada ya ushindi wa 3-2 dhidi ya Brighton na Hove Albion.

Pogba hakuwapo kwa kipindi kikubwa cha msimu wa maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu ya England na United baada ya kukutwa na maambuziki wa virusi vya corona, mwezi uliopita. Kiungo huyo wa kimataifa wa Ufaransa pia hakuwa kwenye kiwango chake wakati 'Mashetani Wekundu' hao wakiibuka na ushindi wa 3-1 dhidi ya Crystal Palace mwishoni mwa wiki iliyopita.

**Pogba alitolewa katika kipindi cha pili dakika ya 65 na alionekana kuwa kama amechoka.**

Na baadaye kocha wa United, Solskjaer alimtetea nyota huyo wa zamani wa Juventus, baada ya Bruno Fernandes kufunga bao la ushindi kwa mkwaju wa penalti.

Penalti hiyo ilitolewa baada ya mwamuzi kujiridhisha kupitia usaidizi wa VAR na hivyo kuwazawadia Man United mkwaju huo.

Baada ya mchezo huo, Solskjaer alisema kuhusu Pogba: "Alikosa mambo mengi wakati wa maandalizi ya msimu mpya kwa sababu alikuwa mgonjwa.

"Hakucheza mechi za kimataifa au mechi ya kirafiki dhidi ya Aston Villa.

"Dakika alizozipata zitamsaidia kuimarika na kuwa bora zaidi."

Katika mchezo huo, Brighton waligonga mwamba mara tano na walionekana kama wangeondoka na pointi moja baada ya Solly March kusawazisha.

Lakini bao la Fernandes likazima matumaini hayo na kuwafanya waondoke uwanjani vichwa chini.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL BADO INAYE AOUAR

KLABU ya Arsenal ipo tayari kuongeza ofa yao kwa pauni milioni tisa zaidi ili kumpata nyota wa Lyon, Houssem Aouar. ***(Football London)***

### CHELSEA WAKOMAA NA RICE




CHELSEA itatuma ofa zaidi ya pauni milioni 40 kwa ajili ya kumsajili, Declan Rice na wanaamini itatosha kupata saini ya kiungo huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 21 kwa sababu klabu yake ya West Ham inahitaji fedha. ***(Sun on Sunday)***

### WEST HAM KWA RUDIGER

WEST Ham inataka kumsajili mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 27 kwa mkopo kutoka Chelsea. ***(Sun on Sunday)***

### LYON YAIKOMALIA ARSENAL




LYON itataka euro milioni 50 kutoka klabu yoyote itakayomhitaji kiungo wa kimataifa wa Ufarabsa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 22, baada ya kuikataa ofa kutoka Arsenal ya euro milioni 36. ***(RMC Sport)***

### BARCA YAMGOMEA FATI

BARCELONA imekataa ofa ya euro milioni 125 ili kumuuza mchezaji wake mwenye umri wa miaka 17, Ansu Fati. ***(Marca - in Spanish)***

### TORREIRA APOTEZEWA TORINO



TORINO haina mpango tena wa kumsajili nyota wa Arsenal, Lucas Torreira na ingawa Atletico Madrid bado wanamhitaji kwa mkopo, 'Washikabunduki' hao wanataka anunuliwe moja kwa moja kiungo huyo mwenye umri wa miaka 24. ***(Football London)***

### UNITED BADO YAMTAKA TELLES

MANCHESTER United bado inapambana kutaka kumsajili mlinzi wa kushoto wa Brazil, Alex Telles - na imeripotiwa kwamba wanajiamini dili hilo la kumtwaa nyota huyo mwenye umri wa miaka 26, linakaribia kufikiwa. ***(Star)***

### INTER YATEGWA KWA KANTE



INTER Milan inajiandaa kuwapa ofa Chelsea ya mlinzi Milan Skriniar mwenye umri wa miaka 25, na kiungo Marcelo Brozovic mwenye miaka 27, ili kumpata kiungo wa kimataifa wa Ufaransa, N'Golo Kante. ***(90 min)***

### FODEN MSHAHARA MNONO

MANCHESTER City inajiandaa kumpa ofa mpya, Phil Foden, ambapo nyota huyo wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 20, ataongezewa mshahara wake wa wiki kwa pauni 30,000 na hivyo kujikuta akiondoka nyumbani na pauni 150,000. ***(90 min)***

### JOVIC KUTOLEWA KWA MKOPO



REAL Madrid inataka kumtoa Luka Jovic kwa mkopo, lakini klabu yake ya zamani ya Eintracht Frankfurt haina mpango na straika huyo wa kimataifa wa Serbia mwenye umri wa miaka 22. ***(AS)***

### LEEDS YAMUWANIA CANTWELL

LEEDS United inajiandaa kutoa ofa kwa ajili ya kumsajili winga wa Norwich City, Todd Cantwell mwenye umri wa miaka 22. ***(Football Insider)***

## Bingwa Ligi ya Wanawake Z'bar ashindwa kupatikana

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MCHEZO wa fainali wa kutafuta bingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar, umeota mbawa baada ya kushindwa kuchezwa kutokana na timu ya New Generations kugoma kuingia uwanjani kuwavaa wapinzani wao Women's Fighter.

Mchezo huo ambao uliopangwa kupigwa juzi, Jumamosi majira ya saa kumi alasiri katika Uwanja wa Mau B, umeshindwa kufanyika kutokana na New Generations kudai wapinzani wao hao, kikosi chao kilijumuisha wachezaji watatu ambao hawakusajili na timu hiyo.

New Generations ilisema wachezaji hao wanacheza klabu za Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara, hivyo hawakuwa halali kuichezea timu hiyo.

Baada ya madai hayo, New Generations walitoka uwanjani wakati Kamishna wa mchezo huo, Mwajuma Juma pamoja na waamuzi wakiwa katika hatua ya kuzikagua kabla ya mechi kuanza.

Akizungumza na gazeti hili Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake Zanzibar (ZFF), Nasra Juma, alisema kamati inasubiri ripoti ya kamisaa Ili iweze kutoa majibu ya kile kilichotokea katika mchezo huo wa mwisho.

Mchezo huo ambao ulivuta mashabiki wengi uwanjani hapo, wanaume kwa wanawake, walilaani kitendo kilichoonyeshwa na timu hizo kwa kushindwa kufuata kanuni. Mmoja wa mashabiki hao, Amina Hassan, alisema timu zote ni kongwe katika medali ya soka la wanawake, hivyo kitendo cha kugomea mchezo huo ni kujitia aibu wao wenyewe pamoja na kutojiamini kama wanaweza katika kupambana.

Aidha, mashabiki wengine walisema wamewavunja moyo hata wanaume ambao walikuwa wapo tayari kuzisaidia timu hizo baada ya kuonyesha msisimko wa kisoka tangu ligi hiyo ilipoanza.

Mgeni rasmi katika mchezo huo alitarajiwa kuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Rizki Pembe Juma, lakini wakati pambano hilo linavunjwa alikuwa bado haijawasili uwanjani hapo.

Hata hivyo, katika mchezo wa saa nane timu ya Jumbi ilifanikiwa kuinyuka Green Queens mabao 13-0, hivyo kumaliza katika nafasi ya tatu ya ligi hiyo.

# MAPRO TISHIO MBIO KIATU LIGI KUU BARA

**Na Mwandishi Wetu**

STRAIKA wa Azam FC, Mzimbabwe Prince Dube, amezidi kupendeza katika mbio za kuwania Kiatu cha Dhahabu Ligi Kuu Bara baada ya kuendelea kuwa kileleni katika orodha ya wafungaji bora akiwa na mabao matatu, kabla ya mechi za jana.

Mzimbabwe huyo, anafuatiwa na 'mapro'/wachezaji wengine kutoka nje ya nchi ambao kila mmoja ana mabao mawili kwa jina lake, Mrundi Bigirimana Blaise wa Namungo FC, kinara wa mabao msimu uliopita, Mnyarwanda Meddie Kagere, Mkongomani Chris Mugalu na Mzambia Claotus Chama wote wa Simba.

Kwa upande wa wazawa ambao nao wameanza kwa kasi katika mbio za kuwania kiatu hicho ni Relients Lusajo, Hassan Kabunda (wote KMC), Marcel Kaheza (Polisi Tanzania) na Mzamiru Yassin wa Simba, kila mmoja akicheka na nyavu mara mbili.

**Msimu uliopita, Kagere alitwaa kiatu kwa mara ya pili mfululizo, ambapo msimu wa 2018/19, alikibeba kwa kucheka na nyavu mara 23 kabla ya msimu uliopita wa 2019/20, kuwa kinara kwa kufunga mara 22.**

Hata hivyo, mabao mawili aliyofunga Kagere msimu huu hadi sasa, yametokana na mechi mbili tu tofauti na Dube ambaye amecheza mechi zote nne za Azam FC akifunga mara mbili dhidi ya Polisi Tanzania wakati wakishinda 2-0, kabla ya Jumamosi kucheka na nyavu kwenye ushindi wa 1-0 walioupata ugenini dhidi ya Tanzania Prisons.

Lakini pia, Mugalu anaonekana anaweza kuwa tishio katika mbio hizo endapo Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, atampa muda zaidi wa kuanza kikosi cha kwanza cha timu hiyo.

Mabao mawili aliyotupia Mugalu, akifunga moja dhidi ya Biashara United wakati wakishinda 4-0 na lingine juzi wakiibuka na ushindi wa 3-0 dhidi ya Gwambina FC, yote Mkongomani huyo alitokea benchi kuchukua nafasi ya Kagere katika dakika ya 76.



Kiungo wa Simba, Luis Miquissone, akipenya katikati ya mabeki wa Gwambina FC katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Mkapa jijini Dar e Salaam juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Tshabalala: Kupaki basi kumeisaidia Gwambina*

**Na Adam Fungwamgo**

NAHODHA msaidizi wa Klabu ya Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala' amesema Gwambina FC imekuwa na bahati ya kutofungwa mabao mengi kama walivyotarajia kutokana na kuja na mkakati wa 'kupaki basi', vinginevyo hali kwao ingekuwa mbaya sana.

Akizungumza baada ya mechi ya Jumamosi, Simba ikichapa Gwambia mabao 3-0 kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Tshabalala aliwapongeza wapinzani wao hao kwa kuwa na mkakati kabambe wa kukaa nyuma ya mpira na kuzuia kwa muda mrefu huku wakifanya mashambulizi ya kushtukiza na hilo kwa kiasi kikubwa jambo ambalo alidai ndilo lililowasaidia, hivyo kuwalazimu watumie mbinu mbadala kusaka mabao.

"Nawapongeza sana Gwambina, wamekuja na 'plan' (mpango) wao wa kutuzuia na hiyo imewasaidia sana, vinginevyo leo hii ingekuwa dhahama, lakini wakatupa wakati mgumu mpaka tukabadilisha mbinu na hata kipindi cha kwanza kilipoisha tukaingia vyumbani, mwalimu akatuambia ni jinsi gani ya kucheza na timu kama hii 'inayopaki basi', ndiyo hivyo ukaona tukabadilika na kushinda," alisema beki huyo wa kushoto.

Nahodha huyo msaidizi, alisema wanachotaka si tu kwamba kila anayekuja Uwanja wa Benjamini Mkapa anafungwa, bali nia yao kubwa ni kuutetea tena ubingwa wao kwa msimu wa nne mfululizo.

Naye Nahodha wa Gwambina, Jacob Massawe, mbali na kuipongeza Simba kwa ushindi huo, alisema walifanya makosa mengi kipindi cha pili na ndiyo yaliyowagharimu.

"Kipindi cha kwanza kama ulivyoona tuliibana sana Simba, na hata goli lao walilipata kwa kosa, ila kipindi cha pili ndipo tulipoanza kufanya makosa mengi, unajua hii timu ni kubwa na ina wachezaji wazuri na wenye uwzoefu, hivyo wanaweza kukusababisha tu ufanye makosa wakayatumia," alisema mchezaji huyo wa zamani wa timu za Stand United na Mwadui FC.

Kwa ushindi huo, Simba inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi 10 na magoli 10 pia.

Gwambina sasa itarejea jijini Mwanza kuikaribisha Ihefu FC Jumamosi, wakati Simba itakuwa na kibarua kigumu Jumapili ugenini itakaposhuka Uwanja wa Jamhuri, Dodoma kuvaava na JKT Tanzania.

# Michezo

Jumatatu Septemba 28, 2020

Nipashe




Solskjaer amchambua Pogba, asema bado UKURASA 22

# Yanga yala miwa Mtibwa kama Kagera

## ●●● Carlinhos mwiba wa mipira iliyokufa, wakiendelea kuokota pointi 3 kwa bao moja...

**Na Somoe Ng'itu,** MOROGORO

KAMA ambavyo ilifanya dhidi ya Kagera Sugar katika mechi iliyopita kwa 'kutafuna mua mmoja' bila majibu kutokana na kushinda 1-0, ndivyo ambavyo Yanga imefanya tena jana baada ya kuibuka na ushindi kama huo dhidi ya ndugu za 'Wakulima wa Miwa', Mtibwa Sugar.

**Katika mechi iliyopita ya Ligi Kuu Bara, Yanga ikiwa Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, iliibuka na ushindi wa bao 1-0 shukurani zikimwendea Mukoko Tonombe aliyeziona nyavu, lakini jana ikiwa dimba la Jamhuri, Morogoro, kona ya Carlos Carlinhos iliyounganishwa nyavuni na Lamine Moro dakika ya 61 ndiyo iliyowapa ushindi.**

Matokeo hayo yanaifanya Yanga licha ya kufikisha alama 10 sawa na watani zao, Simba, kuandamwa na ukame wa mabao kwani haijawahi kushinda zaidi ya bao moja, hivyo kuzidiwa kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa na Wekundu wa Msimbazi.

Katika mchezo wa jana, dakika 45 za kipindi cha kwanza zilimalizika kwa kila upande kushindwa kutikisa nyavu za mwenzake, lakini wageni Yanga wakionekana kuwa na kiu zaidi ya kufunga huku wakicheza zaidi pasi ndefu na mipira ya juu kutokana na uwanja kutokuwa rafiki kwa mipira ya chini.

Beki wa Mtibwa Sugar, Dickson Job alionekana kuwa imara na kuongoza vyema safu ya ulinzi ya timu yake kwa kumzuia mshambuliaji wa Yanga, Michael Sarpong kupeleka mashambulizi kwenye lango lake akishirikiana na Issa Rashid 'Baba Ubaya'.

Dakika ya 11 Carlinhos alipiga krosi nzuri iliyokuwa inaelekea langoni mwa Mtibwa Sugar, lakini Job aliruka kwa ufundi na kuokoa hatari hiyo wakati dakika tano baadaye kipa, Abutwalib Msheri alidaka shuti la Sarpong aliyepokea pasi ya Tuisila Kisinda na kuinyima Yanga bao la mapema.

Job tena aliwahi kutoa nje mpira uliopigwa huku Sarpong akichelewa kuunganisha pasi iliyopigwa kwake na kuwanyima Yanga nafasi nyingine ya kufunga katika mchezo huo uliochezeshwa na mwamuzi, Ludovick Charles kutoka jijini Mwanza.

Msheri akidaka tena shuti la Sarpong dakika ya 29 huku Haroun Chanongo naye aliikosesha Mtibwa Sugar nafasi ya kufunga baada ya shuti lake kuishia mikononi mwa kipa wa Yanga, Metacha Mnata dakika ya 36.

Kisinda alikaribia kuifungia Yanga bao, lakini alikosea kidogo vipimo baada ya shuti alilopiga kupaa langoni dakika 53 huku Job akimdhibiti Carlinhos ndani ya eneo la 18 wakati kipa wake akiwa amepoteza hesabu na kuwanyima wageni hao nafasi nyingine ya kufunga.

**KIINGILIO CHALALAMIKIWA**

Baadhi ya mashabiki wa soka waliofika kushuhudia mchezo huo, walilalamikia uamuzi wa kuweka kiingilio kimoja tu cha Sh. 10,000 ambacho kilipangwa na wenyeji Mtibwa Sugar.

Akizungumza kwa niaba ya wenzake nje ya uwanja, Eddy Joseph, alisema maisha ni magumu na shabiki wa kawaida hawezi kumudu kiingilio hicho wakati mchezo wenyewe hauamui hatima ya ubingwa.

"Wamekimbiza mashabiki na wametukosesha sisi mashabiki wao wa kila siku, Simba alikuja na leo (jana), Yanga ataondoka, atatukosa kwenye mechi zao zilizobakia, kwa kifupi msimu wamemaliza," alisema shabiki huyo.

Kiingilio hicho kilichangia mechi hiyo kuhudhuriwa na mashabiki wachache uwanjani hapo jana tofauti na ilivyokuwa Septemba 12, mwaka huu walipoikaribisha Simba.

***Wakati huo huo***, mashabiki wa Simba kutoka tawi la Mlandizi wakiongozwa na 'Big', waliondolewa na askari wakati wa mapumziko baada ya kudaiwa kufanya fujo.

WANGU HUU...



Winga wa Yanga, Tuisila Kisinda, akiruka na kuuwahi mpira kwa kichwa dhidi ya mchezaji wa Mtibwa Sugar, Baraka Majogoro, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro jana. Yanga ilishinda 1-0. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# Mugalu, Morrison wamvuruga Sven

**Na Saada Akida**

MCHANGO wa dakika za mwisho kutoka kwa watokea benchi, Bernard Morrison ambaye alitoa pasi ya mwisho kwa mfungaji wa bao la tatu, Chris Mugalu wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Gwambina FC juzi, umemwamsha Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, baada ya kueleza hakuna mchezaji mwenye namba ya kudumu katika kikosi cha kwanza.

Morrison aliingia dakika ya 67 kuchukua nafasi ya Rally Bwalya wakati Meddie Kagere aliyefunga bao la kwanza akitoka na Mugalu kuingia dakika ya 75, wakati huo Simba ikiongoza kwa mabao 2-0, la pili likifungwa na Pascal Wawa.

Katika dakika ya 90, Morrison akiwa wingi wa kushoto, alichonga krosi ambayo Mugalu alijaa nayo wavuni na kuiandikia Simba bao la tatu.

Akizungumza viwango vilivyoonyeshwa na timu yake kwa ujumla, Sven aliliambia Nipashe, licha ya wachezaji wake kuonyesha kiwango kizuri, ujumbe wake kwao ni kwamba kila mmoja anapaswa kupambana kuitafuta nafasi hiyo ya kuanza kwa kuwa hadi sasa hakuna mwenye namba ya kudumu.

Kuhusu mshambuliaji Mugalu na Morrison, Sven alisema: "Wamekuwa na mchango mkubwa kwenye timu katika kufanikisha ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Gwambina FC tulioupata."

Sven alisema katika kikosi chake wachezaji wote ni wazuri na wana uwezo mkubwa, na anaamini mwalimu yeyote anatakiwa kuwa na kikosi cha kwanza na wachezaji wa kuanzia benchi.

Alisema ushindani mkubwa uliopo ndani ya kikosi chake katika kila nafasi hasa viungo na washambuliaji, kila mchezaji anatakiwa kuonyesha kiwango kizuri zaidi ili kupambania nafasi ya kucheza kikosi cha kwanza.

"Wachezaji wote wana viwango vizuri, kuanzia anayeanza, aliyekuwa benchi na hata yule ambaye hajavaa jezi, ila kocha anatakiwa kuwa na kikosi cha kwanza watakachoanza, hivyo kila mmoja anatakiwa kupambana kupata nafasi ya kucheza," alisema Sven.

Alisema ameridhishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wake na kwamba mpaka sasa vinampa matumaini ya kufanya vizuri zaidi katika mechi zijazo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >